
# MAJI MAJI



## TOLEO LA KISWAHILI

NA. 10 AGOSTI 1973

### KATIKA TOLEO HILI

ULINZI
WAKULIMA WA MAPINDUZI
SERIKALI ZA KIJESHI - AFRIKA
OPERESHENI CHUNYA
KIWANDA CHA KANDAMBILI
KISWAHILI, MASHAIRI...

UMOJA WA VIJANA WA TANU
WILAYA YA CHUO KIKUU

# MAJI MAJI

AGOSTI 1973 | Na. 10

Hutolewa na
UMOJA WA VIJANA WA TANU
Wilaya ya Chuo Kikuu
S.L.P. 35054
Dar es Salaam
TANZANIA

## KAMATI YA UHARIRI

Ramesh Chauhan
Fratern Minja
Ida Tarimo
Camillus Mahindi
Mwanitu Kagubila
Mugyabuso Mulokozi

## YALIYOMO

| | | Ukurasa |
|---|---|---|
| 1. | TAHARIRI | (ii) |
| 2. | KUTOKA KWA MWENYEKITI | 1 |
| 3. | FIMBO YA MABWANYENYE KUWAPIGIA WAFANYAKAZI — J.K.Kiimbila | 2 |
| 4. | SUALA LA WAKULIMA KATIKA JAMII YA TANZANIA — Walter Bgoya | 5 |
| 5. | MATATIZO YA UJENZI WA UJAMAA TANZANIA | 13 |
| 6. | WASOMI WASIO NA MWAMKO (Otto Rene Castillo) — Mtafsiri: Mwanitu Kagubila | 19 |
| 7. | "KITU ULINZI" -Kapt. A. Shija | 20 |
| 8. | MJADALA WA WAKULIMA WA KIJIJI CHA UJAMAA CHA ISESA — Henry Mapolu | 22 |
| 9. | KUANGUSHWA KWA SERIKALI AFRIKA — J.Mporogoma | 30 |
| 10. | RIPOTI YA SAFARI YA UNGUJA | 34 |
| 11. | RIPOTI YA SAFARI YA CHUNYA, PAMOJA NA MASHAIRI TOKA KWA WAKULIMA WA CHUNYA | 37 |

****************

WAKULIMA NA WAFANYAKAZI WA ULIMWENGU, UNGANENI!
HAMTAPOTEZA KITU ILA MINYORORO YENU!
NA ULIMWENGU WOTE UTAKUWA WENU!

******************

## UJUMBE TOKA KAMATI YA UHARIRI

1. Kamati ya Uhariri inatoa shukrani zake za dhati kwa waandishi wa makala haya na wote waliosaidia katika utoaji wa gazeti hili. Tunatoa shukrani nyingi vile vile kwa Makao Makuu ya Umoja wa Vijana wa TANU kwa kutufyatulia gazeti hili.

2. Gazeti hili la MAJI MAJI litakuwa limetimiza shabaha zake ikiwa litachochea fikra na majadiliano, hasa kuhusu ujenzi wa Ujamaa hapa Tanzania na kwingineko. Hivyo tunakaribisha maandishi kutoka kwa wasomaji wetu kwa ajili ya matoleo yajayo.

3. Mbali na toleo hili la Kiswahili, yapo pia matoleo ya Kiingereza ya gazeti hili hili la MAJI MAJI. Hili ni toleo la kwanza la Kiswahili, lakini si toleo la kwanza la MAJI MAJI. Matoleo ya 1 - 9 yaliandikwa kwa Kiingereza. Halikadhalika matoleo ya 11 - 12 yatakuwa kwa Kiingereza na yatatoka hivi karibuni.

4. Mwisho, tunawakaribisha kwa furaha Ndugu wote wana wa Umoja wa Vijana wa TANU/ASP waliojiunga na chuo hiki kuanzia mwaka huu wa masomo. Hatuna shaka kuwa mtashirikiana nasi katika shughuli zote za kimapinduzi kwa manufaa ya nchi yetu na jamii ya wakulima na wafanyakazi wa dunia nzima. Waswahili husema "Mambo kikowa ndipo yakawa."

*****************

"....Mwingereza anapotaka kuwatumia Watanzania, hawezi kumwendea Msukuma wa hivi hivi tu; haiwezekani. Lazima atawazia wale waliokwisha kupokea mawazo yake, ndio atakaowatumia. Atakwenda mahali ambapo ana hakika kuwa ataungwa mkono, kama vile Chuo Kikuu penye wanafunzi na walimu wanaowapakia mawazo ya kikoloni."

Mwalimu J.K.Nyerere

(Yamedondolewa kutoka <u>Ujamaa ni Imani</u>, uk.

******************

# TAHARIRI

Tunaishi katika enzi za mapinduzi ya ulimwengu. Historia imetutunukia bahati ya kushuhudia mapambazuko ya enzi mpya katika salua ya binadamu: enzi za Uhuru, Amani na Maendeleo, enzi za Ujamaa. Huu ni wakati wa harakati za ukombozi wa wakulima na wafanyakazi w. ulimwengu, ni wakati wa kuasisi jamii mpya katika dunia mpya, ambamo hamna dhuluma, ambamo hamna bwana wala mtwana. Jukumu kuu la kizazi cha sasa cha Afrika, ambalo pia ndio wajibu wa kwanza wa gazeti hili la MAJI MAJI, ni kutoa mchango wake, japo hafifu, katika utekelezaji wa lengo hili kuu la Binadamu.

Ukombozi wa kweli ni ukombozi wa wakulima na wafanyakazi wa ulimwengu kutoka katika nikatale ya ubepari; ukombozi wa Binadamu kutoka katika mahabusu ya mfumo katili wa ubepari na ubepari wa kuhozi. Hapa Afrika huu pia ni ukombozi wa Mwafrika kutoka katika utumwa wa ukoloni na ukoloni-mamboleo. Huu si ukombozi wa kisiasa tu, bali pia ni ukombozi wa kiuchumi; si ukombozi wa kiuchumi tu, bali pia ni ukombozi wa kitamaduni, kiimani, kimawazo.

Lugha kuu ya ukombozi huu ni mishindo ya bunduki. Njia ya kufika kituoni ni nyekundu kwa damu. Lakini lazima kituo kitafikiwa, kwani hakuna marefu yasiyokuwa na ncha. Ncha ya historia nzima ya binadamu, kipeo cha harakati zote za kitabaka za tangu jadi na jadudi, ni kimoja tu: Ujamaa. Hii ndiyo hatima ya kimantiki ya vuguvugu hili.

Dhana hii ndiyo inayozingatiwa katika neno 'Maji Maji'. Vita vya Maji Maji (1905-1907) vilikuwa ni vita vya ukombozi vilivyowajumuisha, kwa mara ya kwanza, Waafrika wa makabila mbalimbali ya Tanzania dhidi ya ukoloni wa Kidachi. Ushinde wa wananchi katika mapambano hayo ulisababishwa hasa na ukosefu wa zana bora za kupigania, achilia mbali itikadi dhaifu iliyoathiriwa na imani za ushirikina. Lakini ikiwa kushindwa kwao kumekuwa ni onyo kwetu sisi vizalia vyao kwamba mapambano yoyote na mabeberu, ili yafaulu, sharti yaimarishwe kwa itikadi safi na silaha bora za kisasa, kukubali kwao kujitoa mhanga kwa ajili ya Uhuru sharti kuwe ni fundisho kwa mabeberu wote kwamba hakuna taifa lolote litakalokiri unyonge wa daima. Kila mdhulumiwa hatimaye hunyanyuka kudai haki zake; na mauti huweza kuwa bora kuliko utumwa wa milele.

Walakini kumwordoa mkoloni siyo hatima ya ukombozi. Kunako magofu ya jamii ya zamani ya kikoloni lazima kuibushwe jamii mpya yenye haki, uhuru na ufanisi. Hii ndiyo fasili ya mchoro ulio katika jalada la gazeti hili. Hatuwezi kujenga jamii mpya ya kijamaa bila kuubadilisha muundo wa kiuchumi. Hii ina maana kwamba, licha ya kuziweka njia kuu za kuzalisha mali katika mikono ya Umma, itabidi vile vile zitumike zana za kisasa katika kilimo ili kuzalisha mali ya kutosha na hivyo kuweka msingi bora wa kuitasini (kuiendeleza kiviwanda) nchi yetu. Hatimaye itabidi upanuzi wa kilimo uende sambamba na upanuzi wa viwanda, Hivyo mambo haya mawili yamefungamana na yanategemeana.

Lakini ujenzi peke yake hautoshi; lazima tukilinde kile tunachokijenga. Mazao ya jasho letu yatatunufaisha iwapo tu yatahifadhiwa dhidi ya maadui ambao daima haweshi mbinu za kutufisidia mambo yetu. Huo ndio umuhimu wa bunduki, kwani hifadhi ya Uhuru na raslimali zetu itatokana tu na "mtutu wa bunduki".

Ingawa lugha ya ukombozi ni mishindo ya bunduki, bunduki hizo hazina budi kutawaliwa na itikadi safi iliyojengwa kwenye misingi ya nadharia ya kisayansi ya Ujamaa. Bunduki peke yake katika utovu wa itikadi safi si silaha kitu katika mapambano haya.

[illegible]

[illegible]

[illegible]

[illegible]

[illegible] ya Chama kukubali lugha ya Taifa.

Lugha ni roho ya taifa na kiongo cha utamaduni wake. [illegible] hai haikosi kuwa na lugha hai, lugha yenye uwezo wa [illegible] kwa ukamilifu [illegible] ya maendeleo ya Umma. [illegible] Tanzania [illegible] lugha ya Watanzania, ambayo ni Kiswahili. Hii ndiyo lugha iliyotumika kuwaunganisha wananchi wote wakati wa kupigania Uhuru; na hii ndiyo lugha [illegible] taifa letu katika ujenzi wa jamii mpya. Kama bado wapo [illegible] wanaoamini kwamba haiwezekani kueleza mambo mazito kwa lugha ya Kiswahili, [illegible] hili la JAJI [illegible] zaidi.

## FIMBO YA MABWANYENYE KUWAPIGA WAFANYAKAZI

na

## JOSEPH KATO KILIMBILA

"Wafanyakazi ni gurudumu la mapinduzi ya kijamaa" - Lenin'.

Mwalimu anapowafundisha wanafunzi darasani hufurahi upeo wa furaha anapong'amua kwamba wanafunzi wake wamemwelewa; anapong'amua kwamba wanafunzi wanatekeleza kwa matendo yale mambo ambayo amewafundisha. Hivyo ndiyo furaha ya mwalimu kwani dalili hizo huonyesha waziwazi kwamba amepanda mbegu njema, yaani hakupoteza nguvu zake. Vivyo hivyo kwa walimu wote wanaofundisha siasa ya TANU - siasa ya Ujamaa na Kujitegemea. Wao hufurahi wanapoona wanafunzi au wananchi wanaanza kufikiri kijamaa, kutenda kijamaa na kusimama imara kutetea imani yao. Na kwa kweli "Imani bila matendo imekufa". Kama wananchi hawaonyeshi kwa matendo kile wanachoamini kisiasa, pengine hatuwezi kuwa na kipimo bora cha kupimia kama yale tuyafundishayo wameyaelewa, wameyaamini, na wanayatekeleza.

Wafanyakazi wa Kiwanda cha Kandambili (Mount Carmel Rubber Factory, Dar es salaam) ni wafanyakazi ambao wamethibitisha katika historia yetu ya ujamaa nchini Tanzania kwamba wako tayari kuifia imani yao ya kijamaa. Wamethibitisha kwamba siasa imeanza kuwaingia. Wamethibitisha kwamba wao wako mbele katika mstari wa mapinduzi. Wametuthibitishia kwamba ile siasa tuliyofundisha-siasa ya MWONGOZO WA TANU wameielewa na imewakaa barabara. Wafanyakazi hao, kwa kifupi, walikata shauri kumpiga teke bepari mnyonya jasho la watu, ajenti wa ukoloni mamboleo na mtetezi wa siasa ya ubepari iliyo dhidi ya Ujamaa. Hilo ndilo jambo waliloamua kutenda. Walitwaa madaraka mikononi mwao; wakajiamulia jambo ambalo waliona linaoana na siasa ya nchi yetu. Waliamua jambo ambalo wanaona litawapa madaraka zaidi na kushirikisha katika uendeshaji wa kiwanda chao, waliamua jambo ambalo ni la kuua ubepari na mfumo wake wa uongozi wa kibepari katika viwanda. Walitaka nini kwa kufanya hivyo? Walitaka kiwanda kinachoongozwa na wafanyakazi wenye sauti na wala si wafanyakazi ambao hawana sauti. Walitaka uongozi wa Kijamaa katika kiwanda, badala ya uongozi wa kibepari. Walitutamkia kwamba wakisha kishika kiwanda uzalishaji wa kiwanda utakuwa maradufu. Walitaka serikali, hususa TANU iwaunge mkono.

Matendo hayo yote ya wafanyakazi 67 yalitufurahisha wengi. Wale ambao hawakufurahi na kitendo hiki ni mabepari na vitimbakwira vyao. Tulianza kuona kwamba hiyo dalili nzuri nchini Tanzania. Ni dalili nzuri kwa sababu kitendo chao ni mazao ya mafundisho ya mwalimu Nyerere kama yanavyoonyeshwa katika Azimio la Arusha na Mwongozo wa TANU.

Haya basi, walipata nini hawa watetezi wa Ujamaa? Walipata n[illegible] walipofuata kwa dhati siasa ya nchi yao? Walipata nini walipojiwek[illegible] mbele katika mstari wa mapinduzi? Walipata nini kwa kugang'ania si[illegible] yao?

Awali walishangiliwa. Hata ndugu Kisumo aliwaunga mkono na watu kadha wa kadha waliwashangilia, walipoona wafanyakazi hawa wa kiwanda cha Kandambili wamehitimu mafundisho yao ya siasa ambayo TANU imewafundisha. Lakini haikupita muda ikabainika waziwazi kwa[illegible] upepo yafaa kuita kimbunga - umewageukia wafanyakazi. Badala ya kimbunga kumkumba bepari - kwa mujibu wa siasa yetu - kikawakumba w[illegible] wa Ujamaa!! Kwa waliofufuka, nambie hiyo ni ishara gani?

Wafanyakazi 67 wakatimuliwa kazini. Ingawa waliiomba erikali iwasaidie sina hakika kama ilivajali. Bila ya ujali imani yao; bila ya kuangalianani aliyewa_undisha hao amaa siasa; bila kuangalia taabu watakazozipata pamoja na watoto ao, jamaa hao wakatandikwa fimbo ya mabwanyenye - wakatimulia kazini. skari wakawatendea kama kwamba watu hawa walikuwa wahalifu. Makomredi akarudishwa makwao na kuonywa washike adabu. Kwa waliokufa na walio-ufuka, nambie hiyo ni ishara gani?

Wafanyakazi walifukuzwa ati hawakuwa na nidhamu. Nidhamu ani? Jamaa hawa waligoma? Jamaa hawa walitukana TANU? Walikosa nini? hambi yao kubwa ni kuwa kwenye mstari wa mbele katika siasa ya jamaa, na kuamka kuliko baadhi ya viongozi wao. Hiyo ndiyo dhambi ao. Kusema kwamba walikosa nidhamu ni kuficha jua kwa ungo. Ni kutu-ia kisingizio cha wapinga maendeleo, ambao baada ya kutolewa WONGOZO tuliwasikia wakisema ati wafanyakazi hawana nidhamu azini. Ni kweli kwamba wakati mwingine wafanyakazi wametumia WONGOZO vibaya, lakini mara nyingi wafanyakazi wamepinga viongozi ao ambao hawawajali au kuwasikiliza wafanyakazi. Hakuna anayeweza ubisha kwamba baadhi ya viongozi ni watu ambao wamejifunzia simamizi wao wa kazi katika nchi za kibepari. Hakuna anayeweza kubisha wamba viongozi wengine wamerithi mtindo wa usimamizi wa kikoloni - tindo wa kutoa amri tu wengine wakaitika "Labeka"! Hakuna nayeweza kubisha kwamba kuna viongozi wengine katika mashirika a.umma ambao hawajasema hata hilo Azimio la Arusha. Walifahamulo uu ya Azimio hilo ni mambo machache wanayosoma kwenye magazeti. ambo mojawapo linaloonyesha ukweli huu ni hili: Unaweza kwenda yumbani kwa kiongozi fulani, usikute hata kitabu chochote juu a siasa yetu. Unachoni vitabu vya uongozi au uchumi - vyote ivyo vikiwa vya kikabaila vitabu ambavyo kiongozi alitumia shuloni nzi za mkoloni,. Je viongozi kama hawa watawezaje kuuelewa uongozi u usimamizi wa kijamaa? wakijuacho hasa ni hiyo ibara ya wongozo inayowapa wafanyakazi nguvu ya kujiamulia mambo yao enyewe. Viongozi kama hao haweshi mgongano na wafanyakazi. anapoona wafanyakazi wameamka, huwaangalia kwa darubini ile ile mbayo mkoloni aliwaangalia "the black poor" "watu wajinga, asiojua chochote, hawana nidhamu. Wahuni hawa, watazame. Wamesoma wongozo, wanautumia vibaya fujo". Badala ya kuwaelimisha kwa ajadiliano marefu, viongozi hao hulia "Nidhamu Wafunze Nidhamu" a wakati mwingine nidhamu wanayolilia si nyingine bali ni ile a kukubali na kutia kila kitu kitokacho mdomoni mwa meneja. akini ile nidhamu ya kijamaa inayowapa madaraka wafanya kazi umhoji meneja juu ya uongozi wake huwa haitakiwi na hao wakubwa. ti hiyo inawapunguzia heshima yao.

Kwa upande wa viongozi kama hawa, wanaowaangalia wafanya kazi kama atu walio na vifufu vya vichwa - vichwa vitupu, visvyo na elimu ala busara - ole wao katika nchi ya Ujamaa! Viongozi hawa wana-a kuelimishwa. Wanapaswa kupewa mafunzo ya kisiasa yenye itika-i ya kijamaa, kwani wasichokuwa nacho ni "busara ya kimapinduzi". wani hawajui kwamba Umma una uwezo wa kutenda mambo ukiamka ki-iasa. Ni Mwenyekiti Mao anayoshikilia jambo hilo, nami naona i hivyo tu. Ya kwamba baadhi ya viongozi walikuwa na mashaka ashaka juu ya uwezo wa wafanya kazi ni jambo lililoonekana wanzoni mwa mgogoro ninaouzungumzia. Wafanya kazi walitamka wamba wakishika kiwanda watakizalisha mara mbili. Lakini ambo lililotolewa na kiongozi mmoja lilikuwa, "Tuna mashaka ama wanaweza kweli kuendesha kiwanda". Maneno kama hayo, ingawa alisemwa na kiongozi mmoja, yanaonyesha utovu wa imani ya viongozi uu ya uwezo wa Umma. Lakini yatupasa kufahamu kwamba Umma ukiamka, ukaelimishwa, unaweza kutenda mambo makubwa.

Sasa tazama tulivyofanya - tumempendelea bepari, kama kwamba diye atakayejenga Ujamaa, na kuwatupa wafanya kazi. Hitilafu ya isiasa iliyoje!! Wafanyakazi kama asemavyo Lenini, ndio gumu-humu ya mapinduzi ya kijamaa. Tazama basi tulivyoua kitovu cha afanya kazi wa kimapinduzi, kitovu ambacho TANU ingekuwa inaji-unia. Yakini TANU ingekuwa na furaha maridhawa kuwa na wafa-yakazi kama hawa ambao ina hakika wamepiga hatua katika mwamko

ya sisa.

Wafanyakazi wa kiwanda cha kandambili walivunja rekodi katika siasa ya Ujamaa nchini Tanzania kwa sababu waliianzisha mtindo wa uongozi ambao ndio hasa unaotakiwa nchini humu: mtindo wa madaraka kutoka chini kwenda juu - kutoka kwa Umma hadi kwa viongozi. Lakini wapinga maendeleo ambao wamerithi mtindo wa kikoloni hawapendi mtindo huu hata kidogo. Wao wakitakacho ni kutoka kwa mtu mmoja kumrisha Umma.

Kuna maswali machache ya kujiuliza kutokana na mgogoro huu: huyu bepari alikuwa na nguvu gani katika tawi la TANU hata akaifanya TANU ikubali wafanyakazi wake watimuliwe? Je, viongozi wanahusikanaje na kiwanda hiki cha Mount Carmel Rubber? Kwa nini serikali haikuona haja ya kukubaliana na wafanyakazi, ikawasaidia kutekeleza siasa ya chama na ikaupiga zii ubepari? Kwa nini ushindi umekwenda kwa bepari?

Kuna pia maswali mengine muhimu ya kujiuliza: NUTA ilifanya nini?Je, kweli NUTA ilikubali wafanyakazi wafukuzwe, na bepari abatizwe kwa maji ya ushindi? Chama kilijadiliana na wafanyakzi kwa muda wa siku ngapi? Ilikujaje Bwana Zimbihile akawaunga mkono wafanyakazi, na baadaye akalazimika kuubadili usemi wake? Ni nguvu gani zilizokuwa nyuma ya Ndugu Kisumo, Ndugu Zimbihile, hata wakaonekana wakibadili kauli zao? Kwa waliokufa na walio-fufuka, hii ni ishara gani?

Kwa vyovyote vile kitendo walichotendewa wafanyakzi wa kiwanda cha kandambili ni kinyumekabisa cha mategemeo yetu. Hakuna anayeweza kukiita kitendo cha mapinduzi isipokuwa kitimbakwira cha mabeberu. Hakika hiki ni kitendo cha kupinga mapinduzi. Kitendo hiki kinatuonyesha kwamba tunapoteza dira katika mapinduzi yetu. Kinatuonyesha kwamba kati yetu kuna watu ambao labda ni adui wa mapinduzi yetu na hawajui msingi wa Ujamaa. Kinatuonyesha kwamba tunahubiri jambo hili na kutenda kinyume chake.

Wakati umefika sasa wa kujisahihisha. Tumekwisha watesa vya kutosha Wazalendo wenzetu. Tunapaswa kujisahihisha, na hakuna kujisahihisha kunakozidi kitendo cha kuwarudisha wafanyakazi wote na kuwalipa mishahara yao yote. Lazima tusimame kwenye kanuni za siasa yetu tulizozijenga lau sivyo tutajaitwa wanafiki wa Ujamaa. Na uwo mwisho wetu kutumia fimbo ya mabwanyenye - itumiwavyo katika nchi za kibepari - kuwapigia wafanyakazi.

=================

# SUALA LA WAKULIMA KATIKA JAMII YA TANZANIA: JUKUMU LAO NA NAFASI YAO KATIKA MAPINDUZI YA KULETA NA KUDUMISHA UJAMAA

na

Walter Bgoya

Wachunguzi wa siasa ya Ujamaa mara nyingi hawakubaliani juu ya nafasi ya tabaka la wakulima katika kuleta mapinduzi ya Ujamaa. Kuna wale ambao wako tayari kuwasahau wakulima na kupendekeza kuwa tabaka la wafanyakazi tu ndilo tabaka la kuleta mapinduzi. Upande mwingine, ukishikilia kuwa kwa sababu tabaka la wakulima ndilo kubwa zaidi kupita lile la wafanyakazi, basi, ni lazima liwe kama uti wa mgongo katika mapambano yoyote ya kuleta Ujamaa. Pande zote mbili hutoa mifano ya historia ya nchi zilizokwisha anza, zikashinda au zikashindwa katika kuleta mapinduzi ya Ujamaa na ni rahisi kwa mtu kuunga mkono upande mmoja kutokana na nguvu ya upande huo kushawishi na kujipatia wafuasi. Lakini je, hii inatosha? Awali ya yote, je kuna tabaka moja tunaloweza kuliita "wakulima" na halina makundi mbali mbali miongozi mwao yenye kuhitilafiana katika maslahi? Kwa mfano katika nchi zą jamii za kikabaila na za kimwinyi kama vile Ethiopia, Burundi ( ambapo bado tabaka la Watutsi linamiliki ardhi na Wahutu ni wapangaji wao) Misri na nchi nyingi za Uarabuni ambako bado Umwinyi umedumu na kuna watu ambao wanaomfanyikia mamwinyi mashambani tunaweza kusema kuwa kuna tabaka la wakulima na tukaweza kujua jinsi litakavyosimama katika mapambano ya matabaka bila kuchunguza kwa undani zaidi migongano ya ndani miongoni mwa hao wakulima. Ni wazi kabisa kuwa mkulima fukara ambaye hana ardhi yoyote na ambaye anauza nguvu zake za kazi kwa kabaila ana fikra tofauti na yule ambaye ana kishamba chake kidogo ijapokuwa hakimtoshelezi mahitaji yake na yale ya familia yake juu ya suala la umilikaji wa ardhi?

Huyu wa kwanza yuko tayari kabisa kuunga mkono utaifishaji na upokonyaji wa ardhi ya makabaila. Wa pili anaweza kuunga mkono ugawanyaji wa ardhi kwa matagemeo kuwa ataongezewa shamba na si ajabu hata kidogo kuwa atapinga utaifishaji na upokonyaji wa ardhi japokuwa fikra hiyo ndiyo ya kimaendeleo na ambayo bila shaka ingemnufaisha yeye kuliko alivyo sasa. Vivyo hivyo kufuatana na ukubwa (pia uzuri wa ardhi aliyonayo mkulima mdogo msimamo wake utakuwa mwingine juu ya maswala ya utaifishaj9 na ugawaji wa ardhi na mapinduzi kwa jumla ya kujenga jamii mpya na uhusiano mpya wa watu katika jamii hiyo.

Tukitazama hapa hapa kwetu Tanzania hasa katika sehemu kama mkoa wa Ziwa Magharibi ambako ukabaila ulikuwa umedumika hata kabla ya ukoloni na pia katika sehemu za Kilimanjaro na Mbeya ambako kwa sababu ya wingi wa watu kwa kila eneo la maili kuna shida ya ardhi tunaona, kwa mfano, kuwa kesi zinazofikishwa mahakamani na migogoro mingi miongoni mwa watu ina msingi ya ugombeaji wa ardhi. Na pia itaonekana wazi kuwa sehemu sehemu hizi zimesita zaidi katika uanzishaji na uendeshaji wa vijiji vya Ujamaa kuliko sehemu nyingine za Tanzania ambazo hazikufikia hatua hii ya ukabaila na umilikaji wa ardhi kibinafsi au kinyumba, kabla na wakati wa ukoloni. Katika sehemu hizi zenye watu wengi zaidi ya ardhi ya kuwatosheleza, tunaona pia kuwa zaidi na zaidi kuna tabaka la watu wachache wenye ardhi na ambao wana nguvu na uwezo zaidi ya wengine kwa sababu ya utajiri unaotokana na kuwa na ardhi hiyo. Ni maana yake kuwa tunakuta kujitokeza kwa matabaka na hisia za ukubwa na mali upande mmoja, na upande mwingine tunaona ufukara zaidi na unyonge na "ufanya kazi au utumishi mashambani kwa wale wasio na ardhi au wenye ardhi ndogo sana.

Tabaka la wakulima kama matabaka mengine yoyote yale lina vikundi mbalimbali ingawaje bila shaka kuna kundi kubwa zaidi miongoni mwa hayo. Hata pale ambapo tuna-fikiria kuwa hapawezi kutokea matabaka miongoni mwa wakulima ( eti kwa sababu kuna mbuga nyingi zisizokuwa na wakazi na kwa hiyo hakuna tatizo la wenye ardhi na wasiokuwa na ardhi) pana haja sana ya uchunguzi.

Ni kweli kabisa kuwa kuna sehemu nyingi zenye rutuba ambako wale wasio na ardhi ya kuwatosha wangeweza kwenda. Lakini inashindwa kwa sababu kwanza nyika hizi haziwezi kutayarishwa kuwa nzuri bila vyombo (ambavyo mafukara hawa hawana) na pia kwa sababu hawana mtaji wa fedha au wa akiba ya vyakula vya kutumia kabla ya kupata mavuno ya kwanza. Kwa hiyo husidi kulundikana katika sehemu ndogo tu ambazo hazitatoshi na hii ni sababu muhimu ya kutoa kwa watu. Kuna sababu nyingine za kimila (sababu zao ambao walitoa na ardhi, hiyo kabla ya kuhamia na walizikwa hapo) na za kijamii kwenda kufungua pori ni jambo la ibu au dalili ya ukabwela-shamba) ambazo zinazuia uanzishaji wa makazi mapya. Mara nyingi hawa wakulima wanashindwa kuhama kwa sababu ni wadeni wa wakulima wakubwa na kwa hiyo wanakuwa "wafungwa" katika vijiji hivyo ambamo hawawezi kupata mahitaji yao ya kuwatosha na ambapo hawawezi kutoka pia.

Ni wazi kuwa chama chetu kitukufu cha TANU na hasa idara yake ya Elimu ya Siasa na Vijiji vya Ujamaa kina jukumu kubwa sana la kuchambua hali halisi ya matabaka katika Tanzania na sababu za migongano mongoni mwa wakulima, migongano ambayo lazima tuielewe katika kutafuta siasa bora ya kuleta mapinduzi vijijini.

Jinsi halisi matabaka yalivyokuwa katika jamii ya Kiafrika hapa Tanzania kabla ya kuja kwa Wakoloni haijulikani vyema. Kuna wale wanaodai kuwa hapakuwa na matabaka na kwamba palikuwa na usawa 'halisi'. Si nia ya makala kupinga au kuunga mkono kauli hii, kwanza kwa sababu hata kama hapakuwa na matabaka ukoloni ulifuzu kiasi cha kutosha kuufanya ubinafsi umiliki kila sehemu ya maisha yetu. Pili uchumi wa fedha badala ya ule wa kubadilishana vitu na umuhimu katika jamii wa fedha kama dalili ya nguvu na uwezo vilihakikisha kwa mara ya mwisho kwamba ushirika wa kiasili wa kuzika na kucheza ngoma utabaki katika insha tu na katika vitabu vya maktaba. Historia hairudi nyuma.

Kazi muhimu ya taifa letu kwa wakati huu ni kujimudu toka kipindi cha maendeleo madogo kabla ya ukoloni na kipindi cha ukoloni kilichovunjilia mbali na kudidimiza zaidi hata yale maendeleo madogo yaliyokuwa yakianza kuchipuka katika jamii yetu. Kufuatana na uchumi wa dunia ulivyo na unyonge wa uchumi wetu imekwisha onyeshwa wazi wazi kuwa wa kibepari hauwezi kuleta maendeleo kwa taifa letu kiuchumi. Azimio la Arusha na Mwongozo wa TANU wa 1971 imetuonyesha dhahiri kuwa taifa letu bado ni shamba la nchi zilizoendelea za Ulaya na uhuru wetu bado ni wa bendera tu. Na hata baada ya kutaifisha benki na vyombo vingine vya uchumi wetu na nchi za kibepari duniani haujabadilika - ni ule wa wanyonyaji na wanyonywao kama inavyodhihirika katika maelezo yafuatayo.

1. Nchi za kibeberu za Ulaya zikiongozwa na Marekani ya Kaskazini, hazikubali uhuru wetu wa Tanzania au wa nchi yoyote nyingine ya Afrika. Na si kwa sababu tu ya kutaka kuendelea kuzinyinya kiuchumi (ijapokuwa hii hasa ndiyo sababu kubwa) lakini pia kwa sababu Uhuru wetu halisi unazuia na kubana hisia zao za ukubwa. Kwa watawala na wanyonyaji wote haitoshi tu kutawala na kunyonya - lazima pia wawe "mabwana wa mabwana" hasa kama mabwana wenyewe ni weupe. Katika historia ya uhusiano wa watu duniani ustaarabu wa Magharibi umekuwa na sifa moja ambayo lazima daima tuikumbuke, nayo ni uharibifu wa jumla wa utamaduni na utu wa wale wote waliopata bahati mbaya ya kukutana nao. Mifano ni mingi - ustaarabu wa Wazungu katika Marekani ya Latina ulifika kiwango cha kutokomeza baadhi ya makabila na kuwatoweshea kabisa kwenye uso wa dunia. Vile vile Bara Hindi, Uchina na nchi nyingine za Mashariki ya Mbali. ustaarabu wa Wazungu haukuwa na nia ya kukubali kujibadilisha au kupokea chochote kutoka katika ustaarabu wa nchi nyingine. La, wazungu wana asili ya uvunjaji wa kila kisicho chao hata kikiwa kizuri. Si ajabu kuwa lengo la mabomu ya Marekani katika Vietnam, Kambodia na Laos ni makanisa, majumba na dalili zote za ustaarabu wa wananchi wa nchi hizo. Katika Afrika, uharabu huu uliendelea tangu zama za kale na hawa wazungu wa karibuni walioleta ukoloni walikuja kusisitiza kuwa Afrika haikuwa na ustaarabu wala utamaduni wowote, ijapokuwa hawakusita kuiba vilivyokuwa na thamani kiuchumi au kiutamaduni na kuvitundika katika majumba yao ya makumbusho huko Uingereza,

Ufaransa, Ubelgiji, Marekani, n.k. Vile walivyoshinda kuvihamisha walivivunjilia mbali, wakitumia bunduki na vitisho kuvunja utamaduni wetu na huku wakitufundisha kuiga utamaduni wao kama vile nyani anavyofundishwa na bwanae. Kwa hiyo leo Wazungu hawana raha kufikiria kuwa dunia yetu nayo inaweza ikajitutumua, ikawa na "uhuru" na kuweka nyenzo halisi za utamaduni wao na utaifa wao. Marekani alijiingiza katika vita vya Vietnam kwa sababu "vijitu vidogo vya manjano" havikuwa na haki ya kuyaadhiri majeshi ya taifa la Wazungu weupe (Wafaransa) katika mapambano ya Dien Bien Phu mwaka 1954. Marekani alitaka kuirudisha hadhi ya Wazungu, na hatuna budi kuwapa heko wananchi wa Vietnam kwa kumtandika na kumwondoa bila hadhi wala hali. Wazungu wana wazimu wa utawala na ubwana juu ya watu wengine.

2. Afrika ya Kusini pamoja na Rhodesia, Namibia na makoloni ya Wareno ya Msumbiji na Angola ni ngome ya mwisho ya ukoloni na ulowezi. Sehemu hii ina maana sana kwa ubepari wa nchi za Magharibi kwa sababu, kwanza, makampuni ya mabepari wakubwa katika sehemu hii yamelimbikiza rasilimali zao na yanachuma faida ya kupindukia (sababu kubwa ikiwa ni kutokuwapo kwa kauli yoyote ya wafanya kazi au serikali kupinga upokonyaji huo), na pili kwa sababu Afrika ya Kusini ni kambi la ubeberu, linalotumika kuvinjaria nchi nyingine za Afrika na katika kuimarisha mbinu za uchokozi kivita katika sehemu hii ya dunia. Kwa hiyo kuamua kupigana na maadui hawa ni kuamua kupigana na dunia nzima ya mabeberu na Tanzania imejiweka katika msitari wa mbele wa mapambano hayo.

3. Uhasama wa nchi za kibeberu dhidi ya Tanzania unatokana na sababu hizi:

(a) Ni nchi mojawapo ya Afrika ambayo imejichagulia na kufafanua msimamo halisi wa kujenga Ujamaa ingawaje siasa hii haijajitenga na kanuni za uchumi wa kibepari duniani na ingawaje bado upinzani wa siasa hii una nguvu (kindanindani) na unasababisha ugumu wa kuitekeleza na mara nyingine kuifanya iende kinyume kabisa na lengo lake. Kwa kufanya hivi na kwa kuchukua hatua (japokuwa za kwanza na japokuwa bado mirija ya ubeberu inanyonya). Tanzania imekuwa "mfano mbaya" na katika mipango ya ubeberu "haina budi ikomeshwe".

(b) Msimamo wa Tanzania wa kuunga mkono vita vya ukombozi vya moto na kukubali kuchukua jukumu la kuwa ngome ya nyuma ya wapiganaji hao wanayoweza kuitumia kwa kushambulia maadui zetu unawatia hofu wakoloni na makaburu na ubeberu wote kwa jumla.

4. Wakulima katika mabara ya Afrika, Asia na Marekani ya Latina tangu ubepari ulipoanza, wamekuwa na uhusiano na mabepari wa nchi za nje, wakitoa mazao ya asili yaliyonunuliwa kwa bei rahisi na mabepari wao kwa matumizi viwandani, na kuwa soko la vitu vilivyotengenezwa tayari toka huko kwa bei aghali sana. Uhusiano huu umemaanisha kuwa daima nchi za Afrika, Asia na Marekani ya Latina zimekuwa ni 'mashamba' ya kuhudumia mahitaji ya mabepari (na wafanya kazi kwa kiasi kidogo zaidi) wa nje. Mgongano uliopo duniani hivi sasa ni ule wa nchi za Afrika, Asia na Marekani ya Latina kutaka kuvunja uhusiano huo usio wa usawa na mabeberu wa Ulaya (na serikali wanazozitawala) wakitumia hila zote na "sheria" za masoko (wanazotunga wao) kudumisha hali hii iliyopo. Matokeo ya mapambano hayo, yaani mapambano ya ukulima wenye lengo la kuuza nje na ukulima wenye lengo la matumizi ya ndani ni vita kali isiyo na huruma wala simile kwa yeyote asiyekubaliana na hali ya hivi sasa.

Hili ni suala gumu sana kwani pamoja na kutaka kujikomboa toka katika uchuuzi unaowapendelea mabepari wa nchi za nje, kuna suala la fedha ya nje inayohitajika sana katika nchi hizi maskini kwa shughuli za ujenzi wa viwanda, upanuzi na utegaji-uchumi katika mikondo mbalimbali ya uchumi wa taifa.

Maswali haya yakiangaliwa kijuujuu hayaelekei kuwa na ufumbuzi na hata yakiangaliwa kwa undani sana ufumbuzi wake si rahisi. Ufumbuzi wake ni vita moja kali, taifa linapojitosa kufa na kupona, na kuzingatia njia moja halisi ya kupindua uhusiano huu na kuwa

........

tayari kupambana na vikwazo vya kila aina mabeberu watakavyoliweka katika jitihadi zao za kuangusha siasa yake ya kujitegemea.

Kama mpaka sasa makala haya hayajafafanua zaidi suala la wakulima katika jamii ya Tanzania na nafasi yao katika kujenga na kudumisha ujamaa siyo kwamba limesahaulika. La hasha. Mpaka sasa makala haya yamejaribu kuonyesha kuwa wakulima katika Tanzania hawako nje ya mfumo wa uchumi wa dunia nzima kwa ujumla uchumi ambao unamgandamiza yeye na unaozidi kudunisha hali yake ingawaje bidii yake katika jitihadi ya kutoa mazao inaongezeka kila mwaka. Yaani anavyoongeza jitihada ndivyo anavyopunguza pato lake. Hapa sina budi kuongeza kuwa uhusiano wa uchumi wa taifa (ambao ni uchumi wa ukulima) unamgandamiza mkulima kwa njia mbili. Njia moja ni ile tuliyokwisha ona - yaani kudidimia kwa bei za mazao yake kutokana na hila za ubeberu na njia ya pili ni ile ya tabaka la watawalamsonge (mabwana-ofisi wasiozalisha mali yoyote ya taifa lakini ambao hupata mishahara mikubwa kutoka katika ziada ipatikanayo kutokana na jasho la wafanyakazi.)

Baada ya uchambuzi huu wa jumla si vigumu hata sasa kuona uhusiano wa wakulima na mapinduzi ya ujamaa katika Tanzania. Suala la kujiuliza na ambalo hatuna budi kulijibu ni hili: je, mkulima ataunga mkono mapinduzi, atayapinga mapinduzi au atakaa tu atazame upepo unakokwenda naye aende huko?

Siasa ya chama cha TANU na uongozi wa Mwalimu Julius K. Nyerere na hatua zinazochukuliwa na Chama na serikali ni za kimapinduzi. Maana ya mapinduzi hapa ni ile inayotolewa na Mwongozo wa TANU (1971), ibara ya 2: "Mapinduzi ni mabadiliko ya haraka katika jamii, mabadiliko ambayo yanawanyang'anya wachache madaraka waliyokuwa wakiyatumia kwa manufaa yao (na ya wanyonyaji wa nje), na kuyaweka madaraka hayo mikononi mwa walio wengi ili kuendeleza maslahi yao". Na "kinyume cha mapinduzi, yaani mabadiliko ya haraka yanayowanyang'anya madaraka wananchi walio wengi, na kuwapa wachache kwa madhumuni ya kuzuia maendeleo ya umma." Wanamapinduzi, inafuata kutokana na maelezo hayo, ni wale wote wanaounga mkono kwa dhati siasa ya mapinduzi; wapinga mapinduzi ni wale wanaopinga siasa hiyo.

Mwongozo wa TANU unatufundisha kuwa"lengo la ukoloni , ukoloni-mamboleo na ubeberu ni kuhakikisha kuwa utajiri wa Afrika unatumika kwa maslahi ya nchi za kibepari za Ulaya na Marekani badala ya kuwanufaisha Waafrika wenyewe." Pia ibara ya 7 inatueleza kinaganaga ni nchi zipi za Ulaya zilizo juu kabisa katika orodha ya maadui wetu. Hata hivyo,(na inaeleweka kwa nini baadhi ya maadui wetu hawakutajwa) ili kuelewa undani wa suala zima la ubepari wa dunia na ubeberu lazima kabisa ieleweke kuwa nchi zote bila kuitoa hata moja, zinazoshiriki katika unyonyaji wa uchumi wa nchi kama zetu (iwe kwa kulimbikiza rasilmali au kwa kutoa mikopo inayochuma zaidi kuliko inavyoongeza mali ya taifa au ati kwa "kushirikiana") hatimaye ni maadui wa nchi yetu. Katika makala marefu ya Dr. Issa G.Shivji ("Mapambano ya kimya-kimya ya Kitabaka katika Tanzania," yaani "The Silent Class Struggle"in Tanzania") ameonyesha waziwazi jinsi mikataba na"ushirikiano"kati ya makampuni yaliyo chini ya Shirika la Taifa la Maendeleo(N.D.C.) na kampuni za kibepari za nje inavyozidi kuimarisha unyonyaji wa kibeberu wa uchumi wa Tanzania. Ukweli wenyewe ni kuwa uchumi kama wa Tanzania uko pembeni lakini ndani ya mswago wa siasa na uchumi wa kibeberu. Kwa hiyo mazingaombwe yoyote wanayofanya wataalam na mashirika ya mabeberu, mathalan Benki ya Dunia, Shirika la Dunia la Fedha, juu ya maendeleo, ushirikiano, mikopo, misaada, na kadhalika havitafuzu chochote kwani bado kiini cha yote hayo ni ubeberu unaoongozwa na Marekani na kutekelezwa na vijibwa vyake (Uingereza, Ufaransa, Ujerumani Magharibi n.k.) katika sehemu mbalimbali ya dunia waliyoigawana.

........

Humu humu nchini mwetu vile vile mna tabaka na makundi ambayo tunayaita maadui kwa sababu ya ushirikiano wao na maadui wakubwa au tuwaite wawakilishaji wa ubepari wa nje tu. Vijinafasi vyao vya kunyonya ni vidogo kwa sababu ya unyonge wao ila hii haina maana kwamba hawana uwezo wa kutekeleza mwenendo wa siasa ya ujamaa kama ilivyoanza kufafanuliwa na chama cha TANU. Ingawaje hapa pia bado hapajafanyiwa uchambuzi halisi ili kujua mapana na marefu ya hisia na vitendo vyao kitabaka, lakini kuna vielelezo vya kutosha vya kutusaidia ni makundi gani na yanachunga maslahi ya tabaka gani.

Azimio la Arusha linasema "nchi yetu ni ya wakulima na wafanya kazi, lakini si nchi ya ujamaa kamili. Ina misingi ya ubebari na ukabaila na vishawishi vyake. Misingi hii ya ubepari na ukabaila yaweza ikapanuka na kuenea." Maelezo hayo juu ya matabaka katika Tanzania ni ya kijumla mno hivi kwamba hayatoshi kuwa msingi halisi wa mbinu za kujenga ujamaa. Tabaka la wafanyakazi linachukuliwa hivi hivi kana kwamba nafasi zao za kazi na mapato yao ni sawa. Tabaka la wafanya biashara na sehemu ya uchumi wa binafsi kwa jumla haijachambuliwa vyema ili kuonyesha tofauti zilizopo na hisia za kitabaka zinazoambatana na makundi hayo. Ni jambo la kushangaza, kwa mfano, wafanyakazi wanapoitwa wanyonyaji wa wakulima na huku wengi wao (81.4% ya wafanyakazi 375,635 katika Tanzania katika mwaka wa 1970) walikuwa wakipata wastani wa Sh. 150 hadi 399 kwa mwezi kwa kufanya kazi saa nyingi sana kuzidi wastani wa saa wanazotumia wakulima shambani. Kama uchambuzi wa kutosha ungefanywa, tungeweza kuona vema ni makundi gani yanayopata mapato makubwa zaidi na ambayo tuna weza kusema hunufaika kwa hali ilivyo sasa kiasi cha kupinga mabadiliko yoyote yenye lengo la kuleta usawa wa mapato katika jamii ya Watanzania. Kwa mfano, ni wazi kabisa kuwa asilimia 4.2 ya wafanyakazi wanaume Tanzania katika serikali kunako mwaka 1970 walikuwa na mshahara wa Sh. 1000 kwa mwezi au zaidi na ambao walipata fungu lenye thamani ya 20% ya jumla ya matumizi yote ya serikali katika mishahara (Sh. 8,313,000 katika Sh. 41,229,739) wana sababu zaidi ya kupinga mabadiliko yoyote ya haraka yanayotaka kubadili hali ya matabaka katika Tanzania. Pia isisahauliwe kwamba hawa huwa ndio hasa wenye kushika hatamu za serikali na ndio hao wanaoamua mbio za utekelezaji wa mipango ya serikali.

Hata hivyo, si nia ya makala haya kutaka kuunda matabaka pale yasipokuwapo ilimradi maelezo yaambatane na msingi wa uchambuzi. Nia ya yote hayo hapo juu ni kusisitiza tu kwamba kuna haja muhimu ya kutafiti zaidi uhusiano wa matabaka katika jamii yetu.

Nimewahi hapo awali, katika utangulizi kusema kuwa kuna wale ambao huzingatia moja kwa moja kuwa tabaka la wafanya kazi ndilo tabaka la wanamapinduzi na siyo lile la wakulima. Mpaka hapa sioni jinsi kauli hii inavyoambatana na hali ya Tanzania na kazi ya muda huu wa mapinduzi yetu. Ingesemekana kuwa wafanyakazi na baadhi ya wasomi wa kimaendeleo ndio wanaotoa uongozi kwa tabaka la wakulima katika mapinduzi ningekubaliana na uchambuzi huu; kwanza, kihistoria (katika Tanzania na Afrika kwa jumla vyama vya wafanyakazi na wafanyakazi maofisini wa kimaendeleo ndio walioongoza vuguvugu la kupinga ukoloni, ngawaje umma wa wakulima ndio uliowatia wasiwasi wakoloni), na pili kwa sababu ya kushiriki kwao katika mapambano ya fikra na nadharia - kutokana na maisha yao ya mijini na kufunguliwa macho na harakati za watu wa nchi nyingine duniani. Ijapokuwa tumeona kuwa hata miongoni mwa wakulima kuna tofauti za maslahi ya makundi mbalimbali napendekeza kuwa hata kama tofauti zingeondolewa (kwa kuzuia uajiri wa wakulima wasio na ardhi katika mashamba makubwa makubwa, na kutaifisha mashamba yote makubwa na kuyafanya vijiji vya ujamaa) bado tatizo kubwa la uzalishaji wa mali litakuwapo, na kuinua hali ya wakulima litabaki ni tatizo kubwa la uchumi wa Tanzania. Sina maana hata kidogo kwamba matatizo ya unyonyaji mashambani hayazuii zinduko halisi la uzalishaji mali wala kwamba kumaliza matatizo hayo kusingesaidia sana katika kuleta maendeleo. La, Nina maana tu kwamba tatizo la ukabaila katika taifa letu ni dogo ukilinganisha na lile la uzalishaji mali kwa jumla.

Hili litaeleweka vyema tukichukua mfano huu. Kwenye mwaka 1960, walowezi wakulima ambao walishika 1% ya ardhi yote ya Tanzania

walikuwa wakizalisha asilimia 50 ya mazao yaliyouzwa nje. Hata kama hali imebadilika sana katika miaka 11 ya Uhuru, sidhani kuwa imebadilika kutosha kuweza kusema kuwa yangechukuliwa mashamba hayo na vijiji au na serikali mazao yangeongezeka kufikia 60% au zaidi ya mazao yote yaliyouzwa nje. Ningedhani kinyume kabisa, yaani mazao yangepungua zaidi.

Tatizo la kujenga ujamaa linatokana kwanza na kuambatana kwa uchumi wetu na mfumo wa ubepari wa dunia unaofanya wakulima kutopata haki ya jasho lao (ziada) kwa sababu ya sheria za masoko zinazobadilikabadilika kila mara kufuatana na maslahi ya ubepari wa dunia; pili, na hili ni muhimu sana, utumiaji mbaya wa hata lile pato dogo tunalopata kitaifa kutokana na jasho la wakulima na wafanya kazi. Kutegemea sana wataalam wa nje wanaoficha ukweli wa hali yetu na ambao huchukua sehemu kubwa ya ziada katika mishahara, majumba ya bure (katika shirika moja dogo la Tanzania, mkurugenzi mmoja mtaalam alikuwa akipata mshahara kwa mwaka ambao ulikuwa nusu ya matumizi ya kuendesha kampuni nzima kwa mwaka mzima na bado akitaka zaidi) na marupurupu mengine mengi.

Kushikilia kwamba matabaka yanayonyonya wakulima na wafanyakazi katika Tanzania ndio msingi wa kutofaulu kwa siasa ya ujamaa katika Tanzania ni suala halali tu [illegible] kama mtu akisema kuwa wale viongozi katika mashirika mbalimbali na serikalili ambao wangeidumisha siasa ya kujitegemea hawafanyi hivyo na wanaipinga (wengine kwa sababu ya kutokujua ni nini hasa kinatakiwa kufanywa) ningekubali.

Katika Tanzania kuna viongozi ambao wanapotosha siasa ya ujamaa kwa sababu ya hisia na maslahi ya tabaka lao la utawalamsonge, na kama katika siku zijazo ukulima ungezidi kupanuka katika mikono ya wachache na viwanda vikazidi kupanuka mikononi mwa mabepari wa ndani na wa nje suala hili lingekuwa la kwanza kabisa. Pia isisahauliwe kuwa kuna kundi la watawalamsonge ambao hupotosha siasa kwa kutoelewa ki-imani lile wanalotakiwa kufanya na ambao wakijiigiza [illegible] wweza kujirekebisha na kutekeleza vyema siasa ya chama.

Kukua na kupanuka kwa matabaka hakutokei katika siku moja. Katika Tanzania katika kipindi hiki cha historia kuna mapambano mawili - moja la kuvunja mianzo ya matabaka ya ndani na kukata mirija ya mabepari wanyonyaji wa nje. Hatuwezi leo kuombolesa kwa kutokuwa na tabaka kubwa la wafanyakazi walioamkuka kisiasa na wenye uwezo wa kuongeza na kusukuma mbele mapinduzi hadi mwisho. Kufanya hivyo vile vile ni dalili ya ndoto na fikra goi goi changa za kibwanyenye hata kama zinajificha katika kauli kali ya mapinduzi. Vile vile hatuwezi kulazimisha kuwapo kwa wakulima mafukara wa chini ambao wame lemewa na unyonyaji wa wakulima wakubwa na ambao wako tayari kunyanyuka katika vuguvugu la maasi ya kimapinduzi wakati jamii yetu si ya kikabaila. Muhimu ni kuichukua jamii yetu ilivyo, tuifanyie uchunguzi kisayansi tukikubali ukweli wa hali iliyopo na huku tukijitayarisha sisi wenyewe na umma wote kwa jumla kubeba mzigo tuliobebeshwa na historia yetu na ya dunia kwa jumla.

Katika historia ya mabadiliko yasiyo halali kikatiba katika nchi za Afrika kama yalivyotokea Ghana, Uganda na sehemu nyingine tunajifunza jambo moja muhimu. Ingawaje katika nchi hizi mbili hasa serikali zilizokuwapo zilikuwa za kimaendeleo (yaani zikiwakilisha maslahi ya umma) wapinga mapinduzi wa kijeshi waliojinyakulia madaraka hawakutwaliwa silaha na wakulima (na wafanyakazi pia ila hapa tunajadili nafasi ya wakulima) na kupingwa hata kuweza kurudisha viongozi halali walioasiwa. Kusema kweli maasi yote katika Afrika yamekuwa maasi ya mijini; ya majeshi (yakishirikiana na tabaka la watalamsonge, ambao vile vile walikuwa wakiiwakilisha maslahi ya mabepari wa nje kupitia kwenye serikali za nchi za kibeberu) na wakulima waneendelea na shughuli zao kama kwamba halikutokea jambo. Katika nchi kulikotokea mapambano ya waasi na wapinga

zikiwa ni kugombea vyeo au ukabila.

Naona kuwa kunas sababu mbili:
1. Kuwa wakulima hawakuona sababu yoyote ya kuunga mkono upande wowote (yaani serikali iliyokuwapo haikuonekana kutekeleza maslahi yao.) na
2. Hawakutayarishwa kutosha kisiasa na kivita - hawakuwa na silaha za kisasa wala mipango yoyote ya kuwaleta pamoja katika mapambano hayo. Hii sababu ya pili ni muhimu sana kwani olo wao wale waliofikiri kwamba "washamba" watanyanyuka na mikuki na virungu kujiingiza katika vita vya watawalamsongo wanaogombea fahari ambayo haiwahusu na kujilaza kama kondoo mbele ya vifaru vya kukopa vinavyolipua mioto ya kienda wazimu.

Kuna njia moja tu ya wakuwavutia wakulima wa chini na wa kati upande wa mapinduzi. Njia hiyo ni kuwatumikia kwa busara na kwa mapenzi. Hili haliwezi kufanyika kama wale wanaokwenda mashambani na vijijini wanakwenda na kasumba ya "uofisa" au kama wanalopata wakulima hawa ni risla tupu zisizoweza kubadili hali ya maisha yao. Hapa lazima tuseme kuwa wakulima hawawezi kuendeleza mbele maisha yao kama hawapativi misaada kama vile vyombo vya kisasa vya ukulima, utaalamu halisi wa kisayansi wenye kuongozwa nasiasa bora ya ujamaa na kujitegemea.

Tumekwisha gusia hapo awali suala la kujitenga na mfumo wa uchumi wa dunia wa kibepari. Wataalam wengine wamesemea sana suala la uchumi wa kijamaa uliosuhubiana kati ya kilimo na viwanda na unaotumia ziada ya shughuli za uchumi siyo katika kujenga majumba ya fahari na mahoteli ya watalii bali katika kununua mbolea na plau za kisasa ambazo peke zinaweza kumsaidia mkulima; na katika kugeuza mashamba yote kuwa vyuo vya uchunguzi wa kisayansi katika ukulima. Si vibaya kwetu kujifunza kutokana na maarifa ya ndugu zetu wa Cuba au Korea katika jambo hili baada ya mapinduzi yao, Kufanya hivi, pamoja na utayarishaji wa wakulima na wananchi wote katika mbinu za ulinzi wa serikali na taifa kutokana na maadui wa nje na wa nadni ndiyo njia pekee ya kuhakikisha kuwa mapinduzi yetu yatafuzu,

Viongozi mwa tabaka la wafanyakazi katika Tanzania, ambao wanaweza wakategemewa kupambana na wapinga mapinduzi hapa kwetu ni wachache sana, na vita vya kisasa vitafyekea mbali viwanda vyao katika siku si nyingi. Si vibaya kujiuliza kwa wakati huu kama wakulima wetu wanaweza kutoa mazao ya kulisha wanajeshi 50,000 mahandakini kwa mwaka mmoja tukifuata kipimo cha mazao wanayotoa sasa. Je, kima hicho cha mazao kinaweza kuchukua uzito wa kupambana na Kaburu? Na mipango gani liyopo sasa ya kubadili hali hii? Pili hatuna budi tujiulize, je wakulima wanatayarishwa vya kutosha kuweza kulinda kwa silaha taifa hili katika vita vyovyote? Au hatujui kuwa tumo vitani? Vita vya kisasa vitakavyokuwa na tumaini la ushindi ni vita vinavyoshirikisha umma wote wa wananchi; vita vyenye kuongozwa na chama cha kimapinduzi, ikiwa lazima kwa muda mrefu sana. Matayarisho ya vita hivyo lazima yaanze kwanza kwa kuweka uchumi mikononi mwa umma, na hili maana yake ni kuongeza mazao na kuyatumia kwa manufaa ya wale wanaoyazalisha.

Hakuna mapinduzi yoyote yanayoweza kufuzu bila ya kuwa na uongozi wa chama cha kimapinduzi, na chama hakiwezi kuwa cha mapinduzi kama uongozi wake katika kiwango chochote hauko mikononi mwa wana-mapinduzi. Kukataa ukweli ni kufumba macho na kukataa kuona, ukabaki kusali tu kuwa lisije lolote la kukupotosha katika njia yako, Hakuna mahali ukweli huu ulipo muhimu kama katika kumudu wakulima kuchukua na kunyanyua juu bendera tukufu ya mapinduzi. Kwa sababu wakulima kwa asili ni wagumu kupokea fikra mpya na kubadili mienendo yao hawana budi kupata uongozi ulio barabara kabisa. Shurti na vitisho havifai chembe kwa wakulima, na ni kwa mifano tu na majadiliano ndipo wanapoweza kushawishika.

Lakini vile vile siasa safi na uongozi bora havitajitokeza katoka mikutano ya hadhara au katika makala nzuri ya wasomi na wataalam, wala havitadondoka kutoka mbinguni kama mvua. Uongozi bora na siasa nzuri vitaumuka katika tanuru la mapambano; mapambano ya vitendo ambavyo hususa ndivyo vinavyotafsiri fikra na hisia kuwa vitu vinavyoshikika na vinavyoonekana. Maendeleo ya mipango ya uchumi, kuunganisha uchumi wa viwandani kutumikia mahitaji ya wakulima na vivyo hivyo uchumi wa wakulima kutumikia mahitaji ya viwanda na wafanyakazi ndiyo njia pekee(na hakuna nyingine) ya kuhakikisha kuwa mapinduzi yako msitari sahihi. Nimekwisha eleza kuwa hili haliwezekani bila kujitoa katika mkondo wa uchumi wa kibepari wa dunia na kutegemea [illegible] nguvu za wananchi wote kwa jumla, nguvu zisizo na kikomo kama ufunguo wa kuondolea mbali matatizo unegunduliwa na kule kusita kwa umma kunakowazuia kuchukua historia na kuitumia kwenda mbele kumekwisha.

Nimejaribu nilivyoweza kuepuka swali hili: "Ni tabaka gani lenye kuleta mapinduzi" kwa sababu jibu langu ni kuwa bila muungano wa umma wa wafanya kazi na wakulima mapinduzi hayawezi kufuzu. Nimedokeza tu kuwa kuna ushahidi wa kutosha kuonyesha kuwa kabla ya ukoloni katika sehemu mbalimbali za Tanzania kulikuwa kumeanza kujitokeza dalili za kuchipuka kwa matabaka. Ukoloni uliendeleza mchipuko huo na kwa kuingiza fedha katika uchumi ukoloni ulizika kwa mara ya mwisho jamii ya Kiafrika isiyokuwa na matabaka.

Nimependekeza vile vile kama walivyofanya ndugu wengine katika maandishi mengi kabla ya makala haya kuwa wakulima si tabaka moja lililoungamika na kuwa kuna makundi miongoni mwa wakulima yenye maslahi tofauti na ambayo hayatakuwa na msimamo mmoja juu ya siasa ya ujamaa. Mfano wa kuzorota kwa jitihada ya ujenzi wa vijiji vya ujamaa katika Mkoa wa Kilimanjaro na matatizo ya Ismani ni ushahidi wa hoja hii. Kwa hiyo ni wazi kuwa uchambuzi wa hali ya mashambani hauna budi ufanywe na siasa na mipango iwange kufuatana na matatizo maalum ya kila sehemu inayohusika.

Hata hivyo mimi binafsi nafikiri kuwa matatizo yanayokabili taifa letu mbele ya yote kabisa ni suala la ulinzi dhidi ya nia mbaya ya mabeberu wakiwatumia vibaraka wao wa humu humu nchini au wakituvamia moja kwa moja (mabomu ya Wareno sasa na Makaburu baadaye) yana uzito zaidi kwa hivi sasa kuliko mapambano ya kitabaka. (ingawaje ninajua vile vile kuwa matayarisho yote haya yanagusian uhusiajo wa matabaka nchini.) Maana yangu ni kwamba wanyonyaji wa ndani wawe ni wakulima wakubwa au mabwana ofisi wanaweza kutengwa na kuvunjwa nguvu kama chama kitazingatia na kueneza siasa yenye msitari wa kutegemea umma kuendesha mapinduzi ya ujamaa.

Uhusiano wa wakulima na wafanyakazi ni uhusiano wa kindugu na matatizo yoyote yanayoweza kutokea kati yao ni yale yaliyo miongoni mwa watu siyo kati ya matabaka mawili yanayogombana. Pili ninakubali uongozi wa tabaka la wafanyakazi katika kueneza siasa ya ujamaa na katika kutengeneza na kuongeza juhudi yao ya kutoa vifaa vinavyohitajiwa na wakulima ili kuongeza uwezo wao wa kuzalisha mali. Sikubali kuwa wafanyakazi ni viongozi na hapo hapo msingi wa mapinduzi. Ni tu umma wa wakulima ulio na uwezo wa kumudu jitihada yoyote ya mapambano marefu ya vita kwa sababu ya wingi wao na kazi yao ya kuwalisha wafanya kazi wa taifa zima. Wao ndio hasa uti wa mgongo, na akiba ya nguvu ya mwisho katika kulinda na kuendeleza mapinduzi.

Mwisho kabisa, mapinduzi ya Tanzania hayawezi kusonga mbele wakati bado siasa ya kujitegemea haijapanuliwa kumaanisha kujitenga na ubepari wa dunia na kutegemea nguvu ya umma wa wananchi kwa jumla. Mipango ya utumizi wa ziada, (ambayo ninaamini hata ilivyo sasa inatosha kabisa kuwa msingi wa kuvunjilia mbali uhusiano na ubepari wa dunia) ni suala la kufa na kupona. Kuzidi kutegemea wema na huruma za nchi zilizoendelea ni kupoteza muda tu, na kuzidi kuwategemea wataalam wa nje ni kuzidi kutia giza na kutia vizibo milipuko ya nguvu za ujenzi walizo nazo wananchi wa Tanzania.

# MATATIZO YA UJENZI WA UJAMAA TANZANIA

Kusherehekewa kumbukumbu ya miaka mia moja tangu kuzaliwa Ndugu V.I. Lenin (kiongozi aliyefuzu katika mapinduzi ya kwanza ya kijamaa ulimwenguni hapo mwaka 1917), pamoja na makala kuhusu maisha yake zilizochapishwa katika magazeti ya hapa nchini Tanzania, lilikuwa ni jambo la maana sana kwetu kutokana na vita vyetu vya kutaka kujenga ujamaa. Kabla ya hapo Lenin na fikra zake nyingi zilikuwa hazitiwi maanani hapa Tanzania. Kusema kweli ilionekana kana kwamba kulikuwa na hila halisi ya kudharau fikra za Marx na Lenin (waanzilishi wa nadharia ya Ujamaa wa kisayansi). Baadhi ya watu hufikiri kuwa fikra za Marx na Lenin ni za kihaini.

Kama ilivyokuwa katika nchi zote zilizokuwa zimetawaliwa na wakoloni, tumerithi hapa Tanzania mawazo ya kikoloni ambayo kusema kweli hayatoweki vichwani mwetu kwa kuondoka tu mkoloni. Elimu aliyotupa ilikuwa na lengo moja tu la kurahisisha jukumu lake la kututawala na kutunyonya. Fikra za Mwalimu katika kijitabu chake cha "Elimu ya Kujitegemea", kwa hivi zilikuja wakati mzuri sana ambapo tuko katika hekaheka ya kuanzisha mpango mpya wa elimu ambayo itatekeleza maslahi ya wananchi kama wao wenyewe na viongozi wao watakavyoamua yatekelezwe. Utambuzi huu wa Mwalimu pamoja na Chama kwamba elimu ina misingi ya kitabaka ilikuwa ni hatua kubwa sana katika mapambano ya kutafuta uhuru wa kweli na kujenga msingi wa utamaduni utakaoambatana na mahitaji ya kimapinduzi ya sasa na baadaye.

Elimu daima ni moja kati ya njia muhimu sana zitumiwazo na tabaka lililoshika hatamu za nchi katika kuzatiti utawala wake. Elimu katika nchi yetu sharti iwe ni njia ya wakulima na wafanyakazi kutawala na kuongoza maendeleo ya kisiasa, kiuchumi, na kijamii katika nchi hii. Yumkini mashirika yote ya kibwanyenye yana jukumu moja la kutekeleza maslahi ya mabwanyenye. Itakuwaje tofauti basi katika nchi ya kijamaa kama si mashirika hayo yatekeleze maslahi ya wakulima na wafanyakazi? Ujamaa ni mpango wa kiuchumi na kisiasa ambapo wakulima na wafanyakazi hutawala mabwanyenye.

Wakati umma wa wakulima na wafanyakazi ulipounga mkono mapambano ya kutafuta uhuru yaliyokuwa yakiongozwa na wasomi, umma huo ulitazamia baada ya uhuru kupatikana yawepo mabadiliko ya kimsingi katika maisha ya kijamii, kisiasa na kiuchumi katika taifa jipya litakalozaliwa. Wakulima na wafanyakazi hawakupigania uhuru ili wapate watawala weusi na huku mambo yote yakibaki vile vile. Walitegemea tabia mpya za viongozi wao. Walitegemea kuwa kutakuwa na uhusiano wa kidemokrasi na wa kiutu zaidi baina yao na viongozi hao (watumishi wa serikali, maofisa wa polisi, mabwana-shamba, n.k.).

Lakini tunajua wazi kuwa mategemeo haya hayakufanikiwa uhuru ulipopatikana, sababu ikiwa ni kwamba mabwanyenye wa Kiafrika walioshika hatamu za nchi baada ya uhuru waliendeleza na mara nyingine hata walizidisha tasvira ya mkoloni aliyekuwa ameondoka na ambaye tayari walikuwa wanamwita arudi kama mtaalam. Mabwanyenye hawa walirithi tabia zile za mkoloni. Walinyakuwa malupulupu yake yale yaliyokuwa ni mali ya mkoloni tu hapo mwanzo.

Kabla ya uhuru, kusema kweli, hakukuwa na mpango mmoja wa elimu katika Tanzania. Kulikuwa na mipango mitatu: moja kwa ajili ya Wazungu, mwingine kwa ajili ya Wahindi, na wa tatu kwa ajili ya Waafrika. Mipango hii si tu kwamba iliwatenganisha binadamu na kuwajaza fikra za kibaguzi kufuatana na rangi, bali pia mambo yaliyofundishwa katika shule hizi tofauti zilizokuwa katika mipango mitatu ndiyo yalikuwa msingi wa kuamua ngazi za kijamii na kiuchumi zitakazokaliwa na watu wa rangi hizo tatu. Matokeo ya jambo hili bado yanaonekana hadi leo hii na tunaweza kutazamia kuwa yatakuwepo kwa muda mrefu ujao. Shule za mamissionari nazo zilipata wafuasi wake pekee, na vile vile zilikuwa na mwelekeo wake tu ambao umeleta matokeo ambayo bado yapo hata hivi leo. Serikali ilitambua ukweli huu ilipoamua mara tu baada ya uhuru kwamba mipango mitatu ya elimu iliyokuwepo ilibidi iunganishwe ili kupunguza na baadaye kufuta kabisa dhuluma iliyoletwa na mipango hiyo mitatu ya elimu nchini Tanzania.

Itakuwa ni ndoto kama tutafikiri kuwa tatizo liliishia hapo. Kuunganisha shule mbali mbali ni suala moja, lakini suala moja, lakini ni suala tofauti kabisa kuzifanya shule hizo ziwe na uongozi na mwelekeo unaofaa ili ziweze kutoa elimu yenye misingi ya kijamaa. Hata hivyo uamuzi wa kuzichukua shule zote ulikuwa ni hatua kubwa sana. Jambo lililo la lazima sasa ni kubadilisha kabisa - kufanya mapinduzi - katika mambo yanayofundishwa katika shule hizi. Ni wazi kabisa kutokana na mambo wanayojifunza wanafunzi wetu pamoja na msimamo wao kuhusu suala la ujamaa kwamba bado tuko mbali sana na lengo la kuzifanya shule zetu zisiwe ni pahali pa kutayarishia maofisia wa kupinga-mapinduzi.

Mabadiliko ya kimsingi yanayotakikana katika elimu yanahitaji mabadiliko makubwa katika falsafa yetu na mawazo yetu kuhusu ulimwengu. Falsafa ambayo yatupasa kuchukua ni ile inayokabili ulimwengu, kwa misingi ya sayansi. Hii ndiyo falsafa pekee inayotambua kanuni zinazofanya ulimwengu usonge mbele, na ndiyo falsafa pekee inayoweza kuzipanga upya kanuni hizo ili ziambatane na misingi ya mapinduzi. Falsafa hii haitumii njia za kuwatisha watu na moto wa ahera, na wala haiwapumbazi watu wasione dhuluma wanayotendewa kwa kuwaahidi kuwa mbingu ni yao. La, hasha! Falsafa hii hujishughulisha tu na mazingara thabiti ya binadamu.

Kutokana na Azimio la Arusha majadiliano kuhusu Ujamaa hapa Tanzania yamefikia kiwango cha juu zaidi kuliko hapo kwanza, na suala lenyewe la ujamaa limewekwa katika msingi mmoja wa wazi hata kama bado ubadilifu unaonekana miongoni mwa watu fulani fulani wanaojaribu kulifafanua. Ambapo hapo kwanza watu walio ... walikana kuwepo kwa matabaka hapa Tanzania na Afrika kwa ujumla, hii leo inakubalika kwa ujumla kuwa matabaka haya yapo na kwamba unyonyaji unaendelea. Inatambulikana pia kuwa unyonyaji ndiyo sababu mojawapo ya umaskini wetu, na hivyo sharti itambulike kuwa njia za kuondoa matatizo yetu ya kiuchumi lazima zitahusiana na kuondoa unyonyaji wa ndani na wa nje pia.

Uwezo wa mapambano yetu kuleta ujamaa hapa Tanzania utategemea jinzi Chama na Serikali vinavyowahi kufagia aina zote za unyonyaji, jinzi vinavyojizatiti na jinzi vinavyokaa macho kufichua hila za ma... beberu ambao wanafunga vibwebwe kurudisha nyuma maendeleo ya nchi na kuwapa hatamu za nchi vibaraka wao.

Sababu zinazofanya uchambuzi wa kisayanzi wa hali thabiti zil... hapa nchini uwe ni wa lazima sana wakati huu ni za wazi kabisa. Azimio la Arusha lilikuwa ni mpango wa kujenga ujamaa katika nchi. Kwa vile Azimio litakuwa ndiyo ngao ya watu wote wa kimapinduzi na wakati huo huo litakuwa ni shabaha ya kuangamiza kwa upande wa wapinga-mapinduzi. Na kujua haya sharti tuchambue kwa kanuni za sayanzi hali ya uchumi ilivyo katika nchi ya Tanzania. Lazima tuwe katika hali ya kuweza kutambua pahali ambapo wakulima fulani ... ardhi ya kutosha (katika vijiji vya kijadi), na lazima tutambue ... milia zipi zina ardhi nyingi kupita mahitaji yake.

Je, kuna uhusiano gani baina ya wakulima maskini, wakulima wa... na wakulima tajiri? Hivi kweli tabaka la wakulima halina migawanyo yoyote na kwa hiyo ni lazima tu ndelee kuandaa mipango ambayo haitofautishi baina ya ngazi mbalimbali za wakulima? Na wafanyakazi je? Ni wengi kiasi gani? Wana uhusiano gani na wakulima? Je, wal... wenye vyeo vya juu katika idara za serikali, mashirika ya taifa na makampuni ya kibepari nao wanasabiwa kuwa ni wafanyakazi? Hivi neno lenyewe "wafanyakazi" linamaanisha nini hapa Tanzania tukifuata mwelekeo wa kijamaa kama tunataka kupata maana ya kimapinduzi ya ... hili? Hivi ni kweli kwamba tarishi ambaye mshahara wake ni shilingi mia mbili kwa mwezi, na ambaye ameweza kupata mkopo wa benki kujenga mabati ya kuezekea nyumba yake ya makuti kwa kuwa hana dhamana, ana maslahi sawa na yule ya meneja wa benki ambaye ana gari inayoendeshwa na dreva wakati wa kazi na usio wa kazi sawia, licha ya hayo ana jumba lake huko Oyster Bay au Isasani na mshahara wake ni shilingi elfu nne kwa mwezi?

Hivi ni vikundi gani vilivyo na motomoto wa mapinduzi zaidi miongoni mwa matabaka haya mawili, na ni vikundi vipi vilivyo na motomoto wa kupinga mapinduzi zaidi? Ni kutokana na vikundi vipi ndipo tutegemee kupata viongozi wetu? Hakuna wakati ambao [illegible] uchambuzi wa namna hii unapaswa kufanyika ili tuweze kupata majibu ya masuala haya yote na tujue ni akina nani walio wanamapinduzi halisi na akina nani walio wapinga mapinduzi kwa sasa au kwa siku za usoni.

Jambo jingine ambalo alijishughulisha sana nalo Ndugu Lenin lili-kuwa ni lile la uofisia (bureaucracy). Katika kijitabu chake kiitwacho "Serikali na Mapinduzi", Lenin aliandika:

"Baada ya kukamata hatamu za nchi, wafanyakazi watavunjilia mbali mjengo uliopo wa kiserikali; watabomoa hadi misingi yake yote, watang'oa kabisa mizizi yake yote, na badala yake watajenga mjengo mpya wa kiserikali ambao utakuwa ni wa wafanyakazi wao wenyewe na watumishi wa ofisini. Ili kuhakikisha kuwa wafanyakazi hawa na watumishi hawa nao hawatageuka na kuwa maofisia, hatua zifuatazo ambazo zilifafanuliwa na Marx na Engels zitachukuliwa bila kusita:

(1) Si tu kwamba kila mtumishi atachaguliwa kwa kura, bali pia ataweza kuondolewa wakati wowote ule;
(2) Mshahara wa kila mtumishi hautazidi ule wa wafanyakazi wa kawaida.
(3) Umma wote utakuwa na madaraka ya kukagua kazi zote za watumishi hawa, na kwa hivi watu wote watakuwa ni 'maofisia' kwa muda na kwa hivi, kwa kweli, hakuna atakayeweza kuwa ofisia".

Makala hii imekusudia kuchunguza masuala matatu aliyoyachambua Lenin pamoja na fikra zake kuhusu masuala hayo kama zinavyohusiana na hali yetu hapa Tanzania. Ni wazi kwamba hatutaweza kulichunguza suala pana la serikali na ujamaa katika makala hii. Hata hivyo jambo la maana ni kuzingatia kwamba wajamaa halisi wote daima wametambua hatari iliyopo katika kuendeleza mjengo wa kiofisia serikalini baada ya mapinduzi ya kijamaa kufaulu.

Katika mazingira yetu, mjengo wa kiserikali tuliorithi ulikuwa ni wa kikoloni. Hatua kadhaa za "kuvunjilia mbali" mjengo huu zimechukuliwa na tunaweza kusema kuwa ushindi fulani umepatikana. Hata hivyo, itakuwa tunajidanganya ikiwa tutafikiri kuwa matatizo yote yanayohusiana na uofisia katika nchi yetu yametatuliwa tayari. Hatari na ubovu uliopo hapa Tanzania kutokana na maofisia wetu hivi sasa ni kama zifuatazo;

(1) Maofisia hawa hawana bidii ya kazi. Suala la bidii, nidhamu, na jitihada ya kujiendeleza mbele katika usomi si wa kazi zao tu bali pia wa elimu ya jumla ni mambo ambayo hayakutiliwa mkazo na mjengo wa kikoloni wa serikali.

(2) Kadiri ujamaa unavyohusika, maofisia hawajui lolote na kwa hiyo hawana hawana uwezo wa kuelewa matatizo ya leo ya kiuchumi; kisiasa na kijamii na wala hawawezi kung'amua njia za kuyatatua.

(3) Maofisia hawa wanaamini kuwa wana haki ya kupata bakshishi na malupulupu mengi bila kujali hali za wananchi wengine zikoje. Jambo hili linakuwa baya zaidi kwa kuwa historia ya maofisia hawa ni ya umaskini na ufukara, na hivyo wanakuwa na ari kubwa ya kujilimbikizia mali ili waweze "kulipiza kisasi" maisha ya taabu waliyoyapata hapo zamani.

Maofisia hawa wanaishi maisha ya anasa, na wanachukia katu fikra zozote za kutaka kupunguza anasa zao ingawa ni wajanja hivi huwezi ukawaona wanapinga ujamaa kimacho-macho. Wanatambua pia kuwa ni sasa tu ndipo maisha yao yamekuwa mazuri sana, na kwamba hakuna pahali pengine ambapo wanaweza kupata raha wazipatazo sasa. Wengi kati ya maofisia hawa sasa ni wazee au basi watu wa makamo, wana wake na watoto kadhaa, na uwezo wao wa kupanda ngazi kiserikali si mkubwa sana. Pia kuna wale vijana wapinga-mapinduzi wakubwa waliotoka katika Chuo Kikuu hivi

karibuni tu, lakini wao mara nyingi inakuwa hawana vyeo vinavyo-waruhusu kukata uamuzi kuhusu masuala muhimu ya nchi, wao mara nyi wana wajibu wa kutekeleza uamuzi uliofanywa na maofisa "wakuu" wao. (4) Maofisia hawa ndio wanaopendwa sana na mabeberu na ni rahisi sana kwao kushiriki, waziwazi au bila wao kujua (mara nyingi bila wao kujua), katika hila za kikoloni mamboleo zinazoendeka hata kila siku na ambazo ni sehemu tu ya njama za kupinga mapinduzi.

Makala hii haina nia ya kupendekeza kwamba serikali iwaondoe moja maofisia hawa tulionao katika mjengo wa kiserikali tuliorithi. Kufanya hivyo ingekuwa ni hatari na kukosa busara. Lakini serikali inapaswa kuzingatia historia ilivyoendeka kuhusiana na mijengo ya kiofisia katika nchi nyingine. Maofisia daima wanakuwa wakifundishwa kuamini kuwa wao ndiyo serikali. Wamefundishwa kuamini kuwa wana siasa ni watu wa matata tu lakini lazima washughulike nao ingawa si lazima wawatii kila wakati. Kwa kuwa kanuni yao ni kwamba mtumishi serikali asijiingize katika siasa, basi wao wanajiona kuwa ni nguzo isiyopendelea upande wowote na inayoongoza jukumu la taifa. Hizi ndizo fikra ambazo maofisia wetu bado wanazo.

Wazo jingine muhimu walilonalo ni kwamba uwezo wa kutekeleza kazi za kiutawala ni muhimu mara kumi kushinda maazimio na mipango yote ya Chama au Baraza la Mawaziri. Wao ni wataalam katika mbinu za migomo-baridi kwani daima huweza kusema kuwa suala aliulizalo mtu linashughulikiwa na idara au sehemu fulani ya serikali, wakati ambapo hakuna mtu yeyote anayelishughulikia tatizo hilo. Maofisia hawa hawana uwezo wa kuangalia mambo kwa msimamo thabiti, daima wao huangalia ni jina la nani lililopo katika kila shughuli. Ukiondoa wale matajiri wa kibinafsi, hawa ndio wenye utajiri mkubwa kuliko watu wote. Kijadi wao ndio tabaka pekee ambao daima wamekuwa na uhakika wa kupata kazi na daima wamekuwa wakitumikia serikali za kipinga-mapinduzi na kugawana nazo utajiri unaoibiwa kutoka katika mikono ya umma wa wakulima na wafanyakazi.

Katika wizara zilizo nyingi, kama si zote, hakuna shughuli za kichama. Uongozi wa wizara uko katika mikono ya mtu mmoja ambaye ana habari na maelezo yote yanayohusiana na wizara hiyo na ambaye hutumia habari na maelezo hayo kuhakikisha kuwa daima anabaki katika cheo hicho. Kama mtu mwenye cheo hicho ni wa kimaendeleo, basi mwelekeo wa wizara hiyo utakuwa ni wa kimaendeleo vile vile. Kama yeye ni mpinga-mapinduzi basi hatua atakazochukua daima zitakuwa za kipinga-mapinduzi. Kwa hivi, ni muhimu sasa hivi kuanza kuweka viongozi wa kisiasa katika wizara na mashirika ya kitaifa, viongozi ambao watakuwa wanafanya kazi kwa niaba ya Chama na serikali na ambao watapitisha kwa pamoja uamuzi kuhusu hatua zinazochukuliwa na wizara baada ya majadilianoya kidemokrasi miongoni mwa maofisa wote wanaohusika.

Baada ya muda makada hawa watapaswa kupendekeza kwenye Chama ni yupi anafaa kuchukua cheo kipi na mapendekezo haya sharti yatokane na kuelewa vyema makada hawa imani ya kila mtu kuhusu ujamaa na uwezo wake wa kufanya kazi. Ni kwa njia hii tu ndipo upinga-mapinduzi wa maofisia utaanza kuvunjiliwa mbali katika jukumu la kupigana na wapinga mapinduzi wote.

Mwisho, swali ambalo lazima tulijibu ni hili: "Chama cha TANU kina wajibu gani katika kuharakisha mapambano ya kumaliza aina zote za unyonyaji, ujenzi wa uchumi thabiti wa kijamaa na ulinzi wa maendeleo yaliyokwisha patikana zidi ya hisia za mabeberu?" Kwanza, chama cha kimapinduzi ni chama cha namna gani? Ni watu gani ndio wanaoweza kuwa katika chama cha namna hii? Kitakuwa na uhusiano gani na serikali? Katika kijitabu kingine kiitwacho "Tuanze wapi", Lenin aliandika kwamba "bila kuwa na mfumo madhubuti, mfumo uliopitia katika mapambano ya kisiasa ya nyakati na mazingira ya kila aina haiwezekani kuwa na mipango thabiti ya shughuli inayoongozwa na kanuni imara na kutekelezwa bila woga, jambo ambalo ndilo pekee linastahili kuitwa mbinu".

Moja kati ya mambo muhimu aliyoongeza Lenin katika nadharia ya ujamaa wa kisayansi ni uwezo wake wa kuandaa mipango pamoja na fikra zake kuhusu mfumo wa chama cha kimapinduzi. Yeye alithibitisha wazi uwezo wake si kwa maneno tu bali hasa katika kukiunda chama cha kikomunisti cha Urusi ambacho kiliweza kuleta mapinduzi ya kwanza ya kijamaa ulimwenguni, alithibitisha kuwa chama lazima kiwe ndicho chombo chenye mwamko wa kisiasa wa juu kushinda watu wote nchini. Sharti kiwe ndiyo ngao ya mstari wa mbele kabisa ya tabaka la wafanyakazi na kiweze kuratibu uhusiano baina ya tabaka hilo na vikundi vingine katika nchi. Chama lazima kiwe na msimamo usiolega lega hata kidogo wa kupinga ubepari kwa maneno na kwa vitendo vile vile, na kiwe katika hali ya kuendeleza mapambano ya kupinga unyonyaji na kujenga ujamaa.

Chama chetu, TANU, kinahitilafiana kimsingi na chama ambacho Lenin aliunda ingawa lengo la vyama vyote viwili ni lile lile la kukomesha ubepari na mjengo wa kijamii unaotokana na ubepari na kujenga jumuia ya kijamaa. Ni nia ya makala hii kuchunguza chama cha TANU kimsingi kadiri iwezekanavyo na kufafanua vipengele vinavyofanya kisiweze kutekeleza vyema lengo hili. Mpaka sasa, yaani tangu vita vya kugombea uhuru, TANU kimekuwa ni chama kilicho wazi kwa watu wote. TANU si chama cha wajamaa au mabepari, si chama cha wafuasi wa nadharia ya ujamaa wa kisayanzi au wafuasi wa nadharia ya kibwanyenye. Ni chama cha wote.

Matokeo ya uwazi huu kwamba misimamo yote ya kisiasa inapatikana miongoni mwa wanachama wa TANU. Ni wazi kwamba hii inamaanisha kuwa ni vigumu kufikia msimamo mmoja wa Chama kwani kitu ambacho mtu angeweza kukiita ni msimamo wa Chama kinatafsiriwa kwa njia tofauti na watu mbalimbali kulingana na maslahi yao mbalimbali. Zaidi ya hayo, na ambalo ni jambo baya zaidi, haiwezekani kuthibitisha kuwa wanachama wote wanafuata mstari wa chama kwani hakuna kipimo cha kupimia imani ya mtu. Nidhamu ya chama haiwezi kuthibitishwa kuwa inafuatwa kwani suala la nidhamu humaanisha kuwa kuna msimamo mmoja au nia moja ya kufuata uongozi. Hata hivyo, suala la kuwa na chama cha kimapinduzi bado halijajadiliwa na TANU yenyewe. Inaonekana kana kwamba mawazo yaliyokubaliwa bila mjadala ni kwamba chama chetu sharti kiendelee kuwa ni chama cha watu wote. Lakini lazima tutambue kuwa ingawa hapo zamani wingi wa wanachama lilikuwa ni jambo kubwa sana katika kupinga ukoloni na kuonyesha Umoja wa Mataifa kwamba wananchi kwa pamoja wamechoka kutawaliwa (kwa kuhesabu tu wale waliopiga kura kupinga ukoloni), wajibu wa chama umebadilika kimsingi sasa.

Mapambano ya sasa ni baina ya wananchi hao hao na wale ambao hawakujiunga na chama hata wakati huo wa ukoloni. Mapambano ya leo ni baina ya wale waliopigania uhuru ili waweze kuwanyonya wananchi (bila kubugudhiwa na mkoloni) kwa upande mmoja, na wale ambao daima wamekuwa wakinyonywa kwa upande mwingine. Kwa hivi ni wazi kabisa kuwa wale wote wanaounga mkono unyonyaji hawastahili kuwa katika chama ambacho kina jukumu la kukomesha unyonyaji. Mawazo ambayo hutolewa mara nyingi, na ambayo hayaridhishi kamwe, ni kwamba TANU lazima kiwe ni chama kinachotetea watu wote. Pia huonekana kuwa ni kwa kufanya watu wote wawakilishwe katika chama tu ndipo wanaweza kujiona kuwa hali zao ni salama na wakatoa mawazo yao bila woga. Kweli, lakini hii ni kukataa kimsingi umuhimu wa tabaka la wafanyakazi na wakulima kuongoza bila shida maendeleo yote ya nchi hii. Kwa maneno mengine, ambapo mabwanyenye wanafanya udikteta dhidi ya wakulima na wafanyakazi katika jamii ya kibepari hatutaki wakulima na wafanyakazi wafanye udikteta dhidi ya mabwanyenye. sasa! Kwani sharti tutambue kuwa ujamaa ni ushindi wa wafanyakazi dhidi ya mabepari. Ujamaa hauwezi kuwa ni muungano wa mabepari na wajamaa!

Mapambano ya kujenga ujamaa yatazidi kuwa magumu kadiri mabepari wanavyozidi kutambua kuwa wanapoteza hatamu za nchi. Kusema kweli ukweli huu tayari umeanza kuonekana. Ingawa Tanzania si nchi ya viwanda vingi na hivyo haina wafanyakazi wengi sana, hata hivyo ni kweli mtupu kwamba wakati chama cha TANU kilipozaliwa hapa mwaka 1954 tabaka la wafanyakazi, likiwakilishwa na vyama mbalimbali vya wafanyakazi na wasomi fulani fulani, ndilo lililoongoza vita vya kugombea uhuru.

Hata kama wakulima waliweka uzito mkubwa katika mapambano haya kutokana na wingi wao, uzito huo ulikuja baadaye kabisa. Jambo ambalo sharti lifanywe hivi sasa ni kutambua umuhimu wa tabaka la wafanyakazi katika kuongoza mapinduzi, na kufanya uchaguzi wenye uangalifu zaidi kufuatana na mwelekeo wa kijamaa katika kuamua ni yupi aruhusiwe kuwa mwana chama wa chama na ni uongozi wa namna gani sharti upatikane katika kuiongoza nchi kuelekea kwenye ujamaa. Si lazima kuivunjilia mbali TANU kama ilivyo hivi sasa, yaani si lazima kuwanyang'anya kadi watu wale ambao tayari wanazo. Lakini TANU lazima iwe na uangalifu wa kimapinduzi katika siku za usoni ili kuhakikisha kuwa wale ambao ni maadui wa ujamaa hawapati nafasi ya kuingia katika chama na kuvuruga mipango yake au basi kutokuendeleza mbele mipango hiyo.

Suala la kuandaa makada wa chama limewahi kujadiliwa na fikra fulani fulani zimepatikana. Ilikubaliwa kuwa makada ni wa lazima kabisa katika mapambano ya sasa katika shughuli zote za taifa: katika uanzishaji wa vijiji vya ujamaa, katika ulinzi, katika kuunda upya mfumo wa kiofisia, n.k., Swali lililosalia ni kama chama kinaliona suala hili kuwa ni muhimu sana au kama wale wanaohusika na utekelezaji wake hawana hakika kama hii ndiyo njia sahihi ya kuimarisha mipango ya chama ili hapo baadaye kiweze kuwa na nidhamu madhubuti katika kujiandaa kuendeleza mbele mapambano.

Imani yetu katika ujamaa inaweza kupimwa kwa kuangalia jinsi tunavyoandaa mipango yetu ya kupigana na ubepari na ukabaila. Kutaifisha njia kuu za uchumi hapa nchini ilikuwa ni hatua kubwa. Lakini haikutosha. Tanzania haikugeuka na kuwa nchi ya kijamaa kutokana na kutaifisha huko. Bado kuna matatizo mengi yanayohitaji ufumbuzi katika kuwaandaa wananchi, hasa vijana, wawe katika mstari sahihi wa imani ya kisiasa. Jambo hili ni gumu sana hasa kwa kuwa bado tuna mashirika mengine ambayo yanaelekeza imani ya vijana wetu katika pande zisizo za kijamaa. Nchi yetu bado inaambiwa isiyaingilie mashirika haya ambayo mara nyingi yana hata njia zake za kueneza propaganda ambamo hufundishia falsafa na imani zake za kipinga mapinduzi. Zaidi ya hayo, mashirika hayo mara kwa mara hujadili masuala ambayo yangepaswa kuachiwa vyombo vya kitaifa. Matokeo yake ni kwamba chama kinagongana na msimamo hii ya mashirika, na vichwa vya vijana wetu haviwezi kuepuka kasumba ya mashirika kama hayo. Ni jambo muhimu sana kwamba vikundi kama hivi ving'olewe mbali au angalau visimamiwe hivi kwamba wawili ni hatari katika kuendeleza ujamaa mbele.

Makala hii imesema hapo awali kwamba Azimio la Arusha ni hatua kubwa na ya juu sana katika mapambano baina ya wanamapinduzi na wapinga-mapinduzi. Hivyo sharti tulizingatie jambo hili na tuwaondolee madaraka wale wote

wanaotaka kuyatumia kwa maslahi ya kipinga-mapinduzi na kuyaweka katika mikono ya wale wenye fikra za kimaendeleo pamoja na makada ambao lazima tuwatayarishe bila kukawia zaidi. Ni wanamapinduzi wa namna hii tu na waliotahiniwa barabara na mazingara ndio wawezao kuunganisha tabaka la wafanyakazi na lile la wakulima. Ni makada hawa ndio wawezao kujiingiza katika pembe zote za uofisia, kung'amua na kufichua yale yatendwayo na maofisia, na hivyo kuanzisha njia za kijamaa za kuendeshea mashirika hayo. Ni makada hawa ndio watakaofanya kazi saa zote bila kulalamika kuhusu hiki na kile kama vile maofisia walalamikavyo kila wakati.

Kufaulu kwa makada hawa pia kutategemea imani isiyolega-lega ya TANU katika jukumu la ujamaa, na jinzi itakavyoandaa mipango na mbinu za kujenga ujamaa.

## WASOMI WASIO NA MWAIKO

Otto Rene Castillo

Siku moja,
wasomi wasio na mwamko,
wa nchi yangu,
watauliza
na wanyonge
kati ya watu wetu.
Wataulizwa walifanya nini,
wakati nchi yao ilipokifa
kama moto mtamu,
mdogo na mpweke.
Hakuna atakaewauliza
kuhusu mavazi yao,
siesta zao ndefu
baada ya chakula cha mchana;
hakuna atakaetaka kujua,
kuhusu jukumu zao mbovu,
zenye 'Wazo lililo tupu'.
Hakuna atakaejali,
ile hali yao ya elimu ya juu.
Hawawezi kuulizwa,
juu ya elimu za ngano za Kigiriki,
au juu ya ghadhabu zao,
wakati mmoja wao
akifa kiwoga.
Hawataulizwa kuhusu
udhihirisho wa vurugu
uliozaliwa katika kivuli
cha uwongo wote.
Siku hiyo,
wanyonge watakuja,
wale ambao hawakuwa na nafasi,
katika vitabu na mashairi
ya wasomi hao,
bali siku zote walitwaliwa
mkate na maziwa,
viazi na mayai,
wale waliowashonea nguo,
wale walioendesha magari yao,
wale waliotunza mbwa na bustani,
na waliowafanyia kazi na
watauliza:
'Ulifanya nini wakati maskini
walipoteswa,
wakati unyonge na maisha
vilipoungua ndani yao?'

Tafsiri ya 'The Apolitical Intellectual'

(Mtafsiri: Mwanitu Kagubilla).

# "KITU ULINZI"

## SEHEMU YA KWANZA

A. Shija

Watu hukaa wakiulizana "Amani itatawala lini ulimwenguni"? Vi... watu wenye imani mbalimbali huomba kutwa na kuchwa kwamba AMANI It... ulimwenguni. Amani ni murua, na tuombao dua la Amani nia yetu ni ... fu lakini basi historia ya walimwengu inatuonyesha kwamba dua peke ... halitoshelezi kuleta Amani; ndio kusema asiyependa shari sharti aji... yarishe kwa shari, ndiyo maana TANU imetamka dhahiri katika MWONGO... kwamba:

"Watanzania tunathamini sana uhuru wa Taifa letu, maana hapo ... unapoanzia ukombozi wetu, na mategemeo ya mapambano ya ukombozi wa ... wananchi wengi wa Afrika. Kwa sababu hii tuna wajibu wa KUCHUKUA ... ZOTE MUHIMU zitakazotuwezesha kuulinda uhuru wetu, ili tuweze kuen... za mapinduzi yetu, na kuifanya nchi yetu kuwa mfano imara wa mapin... ya Afrika."

Yakichukuliwa maanani maneno hayo na kufanyiwa mchanganuo kita... choonekana ni ule ukweli kwamba Ujamaa na Kujitegemea sharti ulind... kutokana na maadui kwa MAKALI ya UPANGA. Ufasaha ya msimamo wetu ... linzi uambatane na matayarisho ya kuhami Tanzania kwa vita vya Umma ... kuamini kwamba tunaweza kuishi kwa amani daima kwamba zipo njia za kukwepa shari za adui zetu wakati ambapo ndipo tumeanza kutekeleza siasa ya Wakulima na Wafanyakazi inayopingana na siasa ya Unyonyaj... wa mabepari, Wakoloni na Vibaraka wao. Badala ya kuhofu mashambulio ... lazima kujitayarisha kwa mashambulio hayo daima kwa sababu adui tun... na wametajwa waziwazi kwenye AZIMIO LA ARUSHA na MWONGOZO kama ifuat...

"Katika upande wa ulinzi wa Taifa, wananchi wawe macho na vibara... waliomo nchini ambao wanaweza kutumiwa na maadui wa nje wenye nia mb... ya kuliangamiza Taifa hili na wawe tayari kulilinda Taifa inapolazim... kufanya hivyo".

Nao Mwongozo Wasema:

"Kwa Tanzania lazima ieleweke kwamba maadui tunaokabiliana nao ana kwa ana ni Ubeberu wa Kiingereza, Ukoloni wa Kireno na Ubaguzi wa rangi wa Makaburu wa Afrika ya Kusini na Rhodesia. Kwa sababu za historia za Jiografia na za siasa mabeberu hawa watakuwa tayari kutushambulia pindi wapatapo nafasi.

Baadhi yetu pengine tungependa kufahamu kwanini uhasama uendelee baina ya Watanzania na Wanyonyaji, sababu kubwa ni kwamba siasa na maslahi yetu na yao vyahitilafiana kimsingi; Watanzania tunayo siasa maslahi ya tabaka la Wafanyakazi na Wakulima, nao Wanyonyaji na Vibaraka wao ni Tabaka kamilifu; mgongano na mapambano baina ya tabaka h... mbili ndio unaotawala uhusiano wa walimwengu leo duniani pote; na hal... hiyo imekuwepo tangu zama za mabwana na Watumwa na Kabaila na Watwa... ambapo leo ugomvi wa kitabaka ni kati ya Mabepari, Wakoloni na Vibara... na Wananchi wanyonywao yaani Wafanyakazi na Wakulima. Akizungumzia juu ya uhasama huu wa kitabaka Mwenyekiti Mao Tse-Tung alisema: "Matabaka yanapigana, baadhi ya matabaka yanafaulu na mengine yanafy... kwa. Hivyo ndivyo ilivyo historia ya Ustaarabu wa maelfu ya miaka".

Nao Mwongozo wa TANU (1971) ulifafanua juu ya hali hii ya mapamba... hayo ni kati ya wale ambao kwa karne nyingi wamekuwa wakinyonya utaj... wa Afrika na kuwatumia wananchi wa Bara hili kama vyombo vyao, kama watumwa wao, na wananchi wa Afrika ambao, baada ya kutambua hali yao unyonge na ya kunyonywa, wameamua kuingia katika mapambano ya kujiko... Mapambano haya ni magumu na ya muda mrefu. Wakati mwingine huwa ya kimya kimya, mara yalipuke kama baruti, wakati mwingine mafanikio hu... kwa wananchi halafu punde si punde mafanikio hayo yakawaponyoka wana... Hivyo ndivyo historia ya Afrika tangu mwaka 1960, ambapo nchi nyingi kiafrika zilijipatia uhuru wao wa bendera. Tangu mwaka huo mpaka le... serikali nyingi halali za Afrika zimeangushwa kwa nguvu, na serikali mpya kuundwa".

Kwa hiyo, leo ni vigumu kutarajia hali ya Amani ambapo Wanyonge ulimwenguni sehemu za Afrika, Asia na Amerika Kusini, ndiyo tu wameanza mapambano ya Ukombozi yenye lengo moja.

Mapinduzi ya Afrika ambapo lengo lake ni ukombozi kamili wa Mwafrika yanapingana na siasa ya Unyonyaji, za ukol ni-Mamboleo na ubeberu. Leengo la Ukoloni, ukoloni Mamboleo na ubeberu ni kuhakikisha kwamba utajiri wa Afrika unatumika kwa masilahi ya nchi za Kibepari za Ulaya na Marekani, badala ya kuwanufaisha Waafrika wenyewe. Kwa hiyo kushiriki katika Mapinduzi ya Afrika ni kushiriki katika mapambano ya kupinga ukoloni na ubeberu.

"Kitu Amani, hali ya shwari ambayo ni tumainio la kila mlimwengu, hakitapatikana mpaka tabaka la Wafanyakazi na wakulima limeshika hatamu za madaraka ulimwenguni pote-yaani ni baada tu ya kuwangamiza mabeberu na wanyonyaji wote ulimwenguni ndipo Amani itakapojengeka na kudumu duniani katika mazingira ya siasa ya Ujamaa na Kujitegemea. Hilo ndilo jukumu la Wafanyakazi na Wakulima Watanzania na walio katika nchi nyingine zinazokabiliana na ubepari na ubeberu.

Dhamira ya makala hii imekuwa kufahamishana jambo moja muhimu: KWAMBA MADHALI TUMEAMUA KULETA MAPINDUZI YA KIJAMAA, kama TANU ilivyoeleza kwenye Azimio la Arusha:
"Tumeonewa kiasi cha kutosha, tumenyonywa kiasi cha kutosha na tumepuuzwa kiasi cha kutosha, Unyonge wetu ndio uliotufanya tuonewe, tunyonywe na kupuuzwa. Sasa tunataka kufanya mapinduzi, mapinduzi ya kuondoa unyonge ili tusionewe tena tusinyonywe tena na wala tusipuuzwe tena", SHERTI VILE VILE KUNG'AMUA KWAMBA TUMEZUA UADUI MKUBWA WA KITABAKA NA WANYONYAJI NA VIBARAKA WAO: LAKINI TUSIFADHAISHWE NA VITENDO VYAO VYA UHASAMA. Kwani adui zetu wanayo sheria moja aliyoielezea Mwenyekiti Mao Tse-Tung kwamba:

"Fanya matata, feli, fanya matata tena, feli tena-mpaka kuangamia kwao, hivi ndivyo zifanyavyo kazi akili za mabeberu na wapinga maendeleo wote duniani katika kupambana na jitihada ya Umma na daima hawatakwenda kinyume na mwendo huu."

Leo swali kubwa siyo kwamba tutashambuliwa au hatutashambuliwa bali ni TUTASHAMBULIWA LINI? Hivyo basi sherti sisi Watanzania daima tujiweke tayari kwa kupambana na adui bila hofu, wasiwasi au woga pindi ashambuliapo; na tuwe na msimamo wa kishujaa kama huo alioieleza kiongozi mmoja shupavu kwamba:

'Pigania, feli pigania tena, feli tena pigana tena-mpaka kushinda kwao; hivi ndivyo zifanyavyo kazi akili za umma.'

Kama walivyosimama imara wakulima na wafanyakazi wa Vietnam na Cambodia kama vile wanavyoendesha mapambano kishupavu wananchi wa Msumbiji, Angola, na Guinea (Bissau); kama vile wakulima na wafanyakazi wa Guinea (Conakry) ya Rais Sekou Toure walivyowaangamiza mabeberu na vibaraka wao; vivyo hivyo Watanzania tusihofu mashambulio ya adui kwani mapinduzi yetu ya Kijamaa yatajengwa kwa jasho na DAMU na madaraka ya Umma yatalindwa kwa MTUTU WA BUNDUKI NA JEMBE.

(Itaendelea katika toleo linalofuata).

# MJADALA NA WAKULIMA WA KIJIJI CHA UJAMAA CHA ISESA WILAYA YA MWANZA

Na

Henry Mapolu

Nilipokuwa katika Wilaya ya Mwanza hivi majuzi, nilipata wasaa wa kuzungumza kirefu sana na wanavijiji katika vijiji vya ujamaa pamoja na watu wengine kuhusu masuala mbali mbali yanyohusiana navijiji vya ujamaa. Mazungumzo hayo niliyanasa katika chombo cha kuchukulia sauti, na kusema kweli yana mafunzo mengi sana yenye manufaa kwani yanaonyesha wazi jinsi watu mbali mbali vijijini wasivyoelewa maana ya vijiji vya ujamaa na jinsi kwa upande mwingine watu wengine - hasa wale walio tayari katika vijiji hivi - tayari wamezingatia maana ya ujamaa na wameamua kutekeleza mipango yao kwa kadiri ya uwezo wao wote.

Natazamia kuchapisha baadhi ya mazungumzo hayo katika matoleo mbali mbali yajayo ya gazeti hili (ikiwa nitaruhusiwa na wahariri) kwani nadhani yanasaidia sana kuelewa kiwango cha mwamko wa kisiasa kilichofikiwa na wananchi.

Katika toleo hili nimechagua kutoa sehemu moja tu ya mazungumzo mengi na marefu niliyokuwanayo na baadhi ya wanakijiji wa kijiji cha ujamaa cha Isesa, Tarafa ya Nkilo. Kijiji hiki kilianza mwezi Januari mwaka 1970, na kwa sasa kina jumla ya wanakijiji 268, watu wazima wakiwa ni 125.

Masuala tuliyozungumza hapa ni matatu tu: suala la mgawanyo wa kazi, suala la upimaji wa kazi, na suala la wanawake katika vijiji vya ujamaa. Nadhani msomaji atagundua wazi kwamba wanavijiji wameongeza sana upeo wao wa mawazo na mwamko wa kisiasa ukilinganisha na wakulima wengine wasio katika vijiji vya ujamaa.

Labda ingefaa niseme machache kuhusu walioshiriki katika mazungumzo haya ili msomaji aweze kujua mawazo yapi yanatoka kwa watu wa aina gani. Bwana H. Lwamgaju, mwenye umri wa miaka 33, ndiye Mwenyekiti wa kijiji na pia Mwenyekiti wa TANU katika Tarafa. Bwana J. Nhalima, mwenye umri wa miaka 39, ndiye mwandishi na mtunza-hazina wa kijiji. Bwana N. Mudodo, mwenye umri wa miaka 35, ndiye Mwenyekiti wa kamati ya kazi katika kijiji. Mabibi Nyanda na Buluba ni akina mama wa makamo - zaidi ya miaka 40 - na wanakijiji wa Isesa. Bi Bertha ni msichana wa umri wa miaka 19, mwanakijiji, na ambaye amemaliza masomo ya msingi hivi karibuni kabla ya kujiunga katika kijiji. Mwisho, Bi Pamba ni Bi Maendeleo aliyetumwa na Idara kufanya kazi katika kijiji hicho.

Nafikiri mkusanyiko huu unawakilisha sehemu zote za mawazo kijijini hapo - kutoka wazee hadi vijana, wanaume hadi wanawake, viongozi hadi wanakijiji, wakulima hadi watumishi wa serikali, waliosoma hadi wasiosoma.

Sasa tuendelee na mazungumzo.

Mapolu: Kuna kazi nyingine hapa kijijini ambazo ninyi huzifanya kwa kufuata saa tu na nyingine mnazifanya kwa kila mtu kupimiwa kiasi fulani. Kwa mfano, kilimo ninyi hukifanya kwa watu wote kulima kwa pamoja tu ambapo uchambuaji wa pamba mnaufanya kwa kila mtu kupimiwa idadi fulani ya madebe. Je, ni utaratibu gani unaofaa zaidi, kufanya kazi kwa pamoja au kupimiana vipimo?

Bi Bertha: Kulima pamoja ni vizuri zaidi, kwani mwingine anaweza kuwa ni mvivu zaidi na hivyo ataachwa nyuma.

Bi Nyanda: Mimi naona ni vizuri zaidi kupimiana miraba, maana katika kulima pamoja tu kuna wengine wavivu: mkilima kidogo anasema anakwenda kunywa maji na wakati atakapokuwa amerudi ninyi mtakuwa mmesonga mbele, mara nyingine atakuwa amekwenda kukaa tu hata maji hakunywa. Lakini kama anajua kuwa ana mraba wake shambani atakwenda kunywa maji haraka-haraka na kurudi kazini bila kukawia.

Bi Buluba: Na mimi naona ni vizuri zaidi kupimiana. Kuna wengine walevi sana, wakati ninyi mnafanya kazi yeye anazubaa-zubaa tu, lakini kama tumepimiana kila mtu atajua kazi yake.

Bi Pamba: Mimi naona njia ya kufuata ni ile inayopendekezwa na wanakijiji, kama wanavyosema kuwa kupimiana ni vizuri zaidi basi mpango huo ni mzuri zaidi. Maana kwa mfano katika uchambuaji wa pamba mtu asipotimiza kiasi chake basi hapati siku. Mtu akijua ana kipimo alichopewa atafanya kazi kwa bidii zaidi ili akitimilize kipimo chake. Kwa hiyo mimi naona kama wanakijiji wangekubaliana kufuata mpango huo katika kilimo pia basi ingekuwa vizuri zaidi.

Bw Mudodo: Mimi pia naona kupimiana ni vizuri zaidi, kwani kuna wengine wavivu, wengine mtafika kazini saa moja unusu lakini yeye atakuja saa mbili unusu halafu mnalipua pamoja. Kwa mpango wa kupimiana mtu anayechelewa kufika shambani basi atachelewa pia kuondoka.

Bw Lwamgaju: Mimi mawazo yangu yanatofautiana na ya wenzangu. Mimi naona kulima kwa pamoja ni vizuri zaidi. Kupimiana kunaweza kumfanya mtu aache kabisa kuhudhuria kazini, maana akishindwa kumaliza kipimo chake kwa siku mbili au tatu mfululizo utaona anaona afadhali kutohudhuria kabisa. Kwa hivi fikra za kufanya kazi kijamaa zitaanza kumtoroka polepole. Kwa hiyo mimi naona kulima kwa pamoja ni vizuri zaidi. Hata ukiangalia tulipofuata utaratibu wa kupimiana katika uvunaji wa pamba, kuna matuta ambayo hayakuweza kuvunwa kabisa kwa sababu ya watu kushindwa kumaliza vipimo vyao; kwa hiyo mpango wa kupimiana hauharakishi kazi kwani pamba bado haijaisha, tungeacha kupimiana nadhani pamba haingesalia shambani kwani wanakijiji wote wangetoka kwenda kuichuma.

Bw Nhalima: Mimi pia naona kulima kwa pamoja ni vizuri zaidi. Kusudi la kuishi pamoja hapa ni kushirikisha nguvu yetu ili mwenye nguvu kidogo aweze kushirikisha nguvu zake kwa wenzake ili wote kwa pamoja waweze kuinuka. Kuna aina nyingi za ushirikiano wa kazi, kwa mfano "kisumba" - ambapo mtu

huenda kufanya kazi pamoja na wenzie mradi afuate tu sheria zilizopo bila kupimiwa kazi, mtu akivunja sheria anapewa adhabu inayolingana na kosa alilofanya. Kwa njia hii watu huweza kufanya kazi kubwa sana, na mimi naunga mkono kwamba kufanya kazi kwa pamoja kunafaa zaidi kuliko kupimiana. Tukipimiana miraba, huenda mimi leo nitamaliza miraba yangu ambapo mwingine atashindwa na itabidi amalizie kesho yake kabla hajapata siku yake. Jambo hili litamfanya aanze kukata tamaa kwa urahisi sana na kuona kuwa maisha yake ni ya kitumwa au ya manamba. Mimi naona utaratibu wa kupimiana sisi bado hatujafikia hatua ya kuuhitaji. Lengo letu ni kuhakikisha kuwa yule mvivu anashirikisha nguvu zake na kuona uzuri wa kufanya kazi kwa pamoja akianza kupata kipato ambacho hapo kwanza alikuwa hakipati. Zaidi ya hayo vijiji vya ujamaa kwa wakati huu vinakabiliwa na matatizo mengi sana, na utaratibu wa kupimiana unaweza kuyazidisha matatizo hayo kwani watu walio nje wataelewa vibaya mipango ya kazi katika vijiji vya ujamaa na watasema kuwa watu wanaojiunga vijijini wanakuwa watumwa wanaopimiwa kila kazi, kwa hivi watu wengi wataanza kuona shaka kujiunga navijiji vyetu.

Bw Lwamgaju: Sasa nadhani ingefaa wale wanaosema inafaa kupimiana nao waeleze sababu zao kwani sasa kuna mashindano kati ya maoni haya mawili. Sisi maelezo yetu tumeyatoa kwa ukamilifu na sasa tuwaachie nafasi wale wanaosema inafaa kupimiana vipimo.

Bi Pamba: Nadhani tutakuwa tunafanya makosa kama tutalichukulia jambo hili kama mashindano, tulichukue tu kama tunapeana mawazo. Nadhani inakubalika kuwa kijiji chetu bado kichanga na kwa hivyo inatupasa kutumia njia za kazi zilizo nzuri kwa kukidumisha kijiji na kuwavuta wale walioko nje ili wazidi kujiunga. Kama lengo ndilo hilo, labda ule mpango wa kulima kwa pamoja unafaa zaidi kwa sasa na hapo baadaye tukisha kukomaa na sisi wenyewe kukubaliana basi hapo ndipo tutapanga utaratibu wa kupimiana kazi. Kwa sasa nadhani ingefaa tuendelee na utaratibu wa kulima kwa pamoja.

Mapolu: Hivi kwa nini mlianzisha huu utaratibu wa kupimiana madebe katika uchambuaji wa pamba?

Bw Mudodo: Tuliona kuwa tunachelewa katika kazi hiyo ya kuvuna pamba na pia katika kuichambua; kwa hiyo tukaona afadhali kila mtu apimiwe kiwango, na hapo tukaona kuwa kazi inakwenda haraka zaidi. Kwa kweli kupimiana kunaharakisha kazi kwani kama unavyoona sasa tumemaliza kuchambua pamba, ingekuwa tunachambua tu hivi hivi hata sasa tungekuwa bado hatujamaliza.

Bi Pamba: Kwa kweli mimi sipingani na lile wazo la kupimiana, lakini inavyoonekana ni kwamba kwa kuwa kijiji bado ni kichanga utaratibu wa kufanya kazi kwa pamoja unavutia zaidi. Lakini labda baadaye wanakijiji wamekuja kuona kuwa kufanya kazi kwa holela kunamruhusu mtu kuja kazini wakati wowote na hivyo kunamfanya afanye kazi kidogo tu. Kwa hiyo labda kutokana na uvivu wa baadhi ya wanakijiji ndio uamuzi wa kupimiana madebe ukapitishwa. Kwa hiyo kwa sasa jambo la kufuata ni kwamba kamati ya kazi ijitahidi kuwashauri wale wanaoonyesha uvivu na kuwaelekeza umuhimu wa

k kufanya kazi kwa bidii.

Mapolu: Mwenyekiti wa kijiji, unakubaliana na wazo kwamba kupimiana kunaharakisha kazi ya kuchambua na kuvuna pamba?

Bw Lwangaju: Kazi ya kupimiana katika kuchambua pamba na katika kilimo ni tofauti; katika kilimo kupimiana kutaleta sura mbaya sana. Kazi ya kuchambua pamba inafanywa na watu walioketi na kuzungumza tu kivulini, lakini katika kilimo kupimiana kutamaanisha mtu anapewa kipande kabisa na hapati siku mpaka amekimaliza. Maana hata nyumbani kama jamii zikianza kupimiana kazi, baba umalize hapa, mama pale, mtoto pale, basi picha itakayotoka ni ile ya manamba kama ilivyokuwa wakati wa ukoloni watu walipokuwa wanaandikishwa manamba. Kwa sababu hii sisi tumeona kuwa katika kilimo mpango mzuri ni sisi sote kulima tu kwa pamoja, na kamati ya kazi ikiwa imara kama ilivyo sasa basi tunaweza kulima ekari nyingi sana bila shida yoyote.

Mapolu: Labda sasa tuendelee na jambo jingine. Kusudi la vijiji vya ujamaa ni kila mtu apate pato kutokana na jasho lake. Ndiyo maana tunaona hata akina mama wanakuwa wanakijiji na kupata siku zao wao wenyewe badala ya kutegemea kazi ya baba mwenye nyumba tu. Kwa hivi mama naye anapata pato lake mwenyewe kutegemea kazi anayofanya. Lakini je, labda wanawake wanapunjwa kwani wao wanakwenda kulima sawasawa na wanaume lakini inawapasa pia wafanye kazi za nyumbani kama vile kupika na kuangalia watoto. Kwa hivi siku nyingine mama anaweza kukosa siku kwa kuwa mtoto analia sana, au kuna wageni na inampasa awatayarishie chakula. Lakini baba yeye anapata siku kama kawaida. Kwa hivi inaonekana wanawake wanapunjwa, kwani ikiwa mwanamke atapata siku sawa na mwanaume itamaanisha kuwa amefanya kazi zaidi kuliko mwanaume, lakini kwa kawaida mwanamke atapata pato dogo zaidi kwa sababu kazi zake ni nyingi zaidi.

Bi Nyanda: Kwa kweli sisi wanawake tuna kazi nyingi sana. Mara nyingi asubuhi itanipasa kuamka mapema kwenda kuchota maji, halafu nitayarishe chakula cha watoto, halafu pengine mtoto atakuwa analia na hivyo itanilazimu niondoke shambani mapema na hapo labda mgeni atafika. Inawezekana niende kuomba ruhusa kwamba nina wageni, huko nitaulizwa kwa nini sikufika upesi kazini na nitaeleza kuwa mtoto alikuwa analia. Inawezekana ruhusa sitapewa na mimi kwa kuwa nina wageni na inanipasa niwatafutie chakula nitaondoka tu na kupoteza siku. Kwa hiyo sisi tuna kazi nyingi zaidi; ni kweli wanaume wanafanya kazi kwa bidii lakini hata mimi tukikutana shambani nitafanya sawa tu nao ingawaje mimi ni mzee, lakini ukiangalia shughuli zangu za watoto na chakula, hapo inakuwa vigumu kwangu kutimiza kazi za shamba sawa na wanaume.

Bi Buluba: Ni kweli sisi wanawake tuna kazi nyingi, lakini kama hivyo ndivyo, basi inatupasa kujitahidi kuamka mapema na kuzitekeleza zile kazi za nyumbani mapema kabla ya kwenda shambani. Kama nina mgeni sharti nikaombe ruhusa, lakini kwenye kazi za ujamaa ni wajibu wangu kufika.

Bi Bertha: Mimi ninavyoona ni kwamba sisi wanawake

Bi Bertha: Mimi ninavyoona ni kwamba sisi wanawake inatupasa kwanza tufanya kazi za nyumbani asubuhi na mapema halafu tuende shambani, kama kuna shida nyumbani basi taarifa inakwenda kwa Mwenyeji wa Kazi, akikubali narudi nyumbani kutimiza shida zangu. Lakini wanaume na wanawake hatupunjani, wote tuko sawa tu. Hata wanaume nao wana kazi za nyumbani.

Bi. Panba: Mimi nadhani inaeleweka kwa ujumla kuwa shughuli za wanawake ni nyingi kuliko za wanaume, ndiyo maana imesemekana kuwa katika vijiji vya ujamaa sharti kuwepo kituo cha watoto wadogo amb watoto wataangaliwa na mtu maalum wakati wazazi kazini; hata hivyo kwa upande wa shida za nyumba nadhani hizo lazima ziwaelemee akina-mama. Na kama mtoto ni mgonjwa basi mama anaruhusiwa kuba nyumbani kwani inakuwa sawa kama baba ambaye naye anaweza kuugua na akabaki nyumbani.

Bw Lwamgaju: Mimi naona kuwa katika vijiji vya ujamaa wanawake wanapunjwa hasa kwa kuwa vijiji hivi bado ni vichanga. Kwa mfano shughuli ya uleaji wa watoto inawapa taabu sana akina mama kwani inawapasa kila wakati waache kazi za kijiji kwenda kumwangalia mtoto na mara nyingi atatafuta kisingizio ili aweze kurudi nyumbani kumwangalia mtoto. Kwa hivi wanawake wanapunjwa kwa ajili ya kukosekana vituo vya kulea watoto. Kwa upande wa magonjwa, shida hiyo inatokana na kutopatikana kwa mapato makubwa, kwani kama ingewezekana magonjwa yote yanget ibiwa kwa ghara za kijiji na mama aliyekosa siku kwa ajili ya kutunza mtoto wake mgonjwa naye apate pato kama vile angekuwa amehudhuria tu. Kwa hiyo kwa siku zijazo nadhani itafaa kama kijiji kitakuwa na fungu la shida kama hizi. Kwa ujumla basi mimi nakubaliana kuwa akina mama wanapunjwa kwa ajili ya kukosekana kituo cha kulelea watoto. Akina baba sisi tunafanya kazi za shamba tu, na tukisha kurudi au tunacheza karata au kwenda kwenye pombe kweli tunaweza kushughulika na ujenzi wa nyumba, lakini hiyo ni kazi ya muda; lakini mama kila siku ana kazi nyingi sana. Ingekuwa kuna kituo cha kulea watoto wote, halafu kukawa na watu wanaoshughulika na utayarishaji wa chakula cha wanakijiji wote ili wakitoka kazini kila mtu anapimiwa uji, basi kazi za akina mama zingepungu

Bw Nhalima: Kuhusu suala hili la akina mama nadhani inaeleweka wazi kwamba akina mama wanapunjika sana. Kwa kweli hata kama kungekuwa na kituo cha kulea watoto, bado kunakuwepo shughuli nyingi za nyumbani ambazo inawapasa wazitimize, kwa hivi shughuli zao kwa kweli ni nyingi sana. Mimi asubuhi nikiamka najua kwenda shambani tu, lakini mama itambidi aangalie kwanza shughuli za kuteka maji, kukogesha watoto, kutayarisha chakula, na shida nyingine za nyumbani. Kwa hiyo ni jambo la lazima sana mipango itafutwe ya kuwapunguzia mzigo huu akina mama, kwani tulipoanzisha kijiji cha ujamaa tulikuwa na kusudi la kuhakikisha kuwa kila mtu ananufaika kutokana na jasho lake. Kwa jumla basi maoni yangu ni kwamba akina mama wanapunjika.

Mapolu: Je kwa upande wa chakula cha akina baba: inafaa kila nyumba ijipikie au labda kungekuwa na chakula cha pamoja kwani huenda ikawa nampunja mke wangu ikiwa itampasa kunipikia mimi pindi tukirudi kutoka kazini?

Lwa
<u>Bw Lwamgaju</u>: Mimi naona chakula nacho kipikwe cha pamoja pia kwani hapo ndipo tutapata kupumzika. Inafaa kukaa na utaratibu kwamba watu wawili wanapewa siku kwa ajili ya kupika chakula cha wote tu ili tukirudi kazini sote tunafika kula na baada ya hapo kama tunapenda kucheza karata au kusikiliza radio basi sote tunakaa. Kwa hivi mama naye atakuwa na uhuru, kuliko sasa inampasa atoke shambani halafu aanze kutafuta kuni, kuchota maji na kupika chakula wakati mimi napumzika tu. Kwa hiyo inafaa sote chakula kiwe cha pamoja.

<u>Mapolu</u>: Basi tuende kwenye suala jingine. Katika mgawanyo wa kazi, watu mbali mbali wanapewa kazi mbali mbali. Wengine wanachambua pamba, wengine wanauza vitu dukani, wengine wanashona cherehani, na kadhalika. Labda inawezekana kuwa kuna kazi nyingine ambazo ni ngumu zaidi na hivyo zingestahili thamani kubwa zaidi; kwa mfano kazi fulani inaweza kuwa na thamani ya nusu siku, kazi nyingine siku moja, kazi nyingine siku moja unusu, na vivyo hivyo. Je, utaratibu huu unafaa au unaofaa ni ule wa kuipatia kila kazi thamani sawa tu?

Nya
<u>Bi Nyanda</u>: Kama mtu mmoja amepewa kazi ya kutengeneza hesabu za kijiji, basi naye anashughulika kama wanavyoshughulika wanakijiji wengine tu na hivyo itapasa apate siku sawa na hao wengine. Hata kama kungekuwa na kazi kubwa namna gani sharti ipewe siku ile ile moja tu kwa kila kazi.

<u>Bi Bertha</u>: Mimi ninavyoona ingefaa waanze kwanza kuzungumza wanaume halafu sisi tutazungumza baadaye.

<u>Bw Lwamgaju</u>: Lakini si tulisema kuwa hapa hatuna mashindano kwa hiyo kila mtu anatoa mawazo yake tu?

<u>Bi Pamba</u>: Mimi pia naona waanze wanaume kwanza kusema.

<u>Bw Mudodo</u>: Lazima wanawake wamalize kwanza mawazo yao ndiyo na sisi tutasema.

<u>Bi Bertha</u>: Si kwamba hatutaki kutoa mawazo yetu, wao wazungumze kwanza halafu na sisi tutatoa mawazo yetu.

<u>Bw Mudodo</u>: Lazima wanawake waseme kwanza kwani kama sisi wanaume tukisema kwanza wanawake hao watafuata yale yale tunayosema sisi.

<u>Bi Bertha</u>: Hapana, hatuwezi kufuata; kila mtu ana mawazo yake tu.

<u>Bw Lwamgaju</u>: Lakini katika kijiji kuna kazi gani ngumu na kazi ipi rahisi? Mimi naona kama ungefafanua hapo ndipo swali lako lingekuwa rahisi zaidi.

<u>Mapolu</u>: Hapa sizungumzii juu ya Iasa, nazungumza kijumla tu. Katika vijiji vingine vilivyoendelea zaidi na vina shughuli za kiuchumi nyingi zaidi,

utakuta kwa siku moja aina nyingi sana za kazi zinafanywa na watu mbali mbali. Kwa hivi kuna kuwa na tatizo kwamba watu wengine wanagombea kazi fulani wanazoona ni rahisi zaidi, kwa hiyo kijiji husipanga kazi zote na kuziwekea thamani tofauti. Kwa hivi mtu ana uhuru wa kuchagua kazi rahisi au ngumu akijua kuwa thamani yake itapitana na thamani ya kazi zinazofanywa na wengine.

Bw Lwamgaju: Seremala anapofanya useremala wake anatumia ujuzi na kwa hiyo hakuna ubaya kama yeye akipata siku sawa na yule anayeuza vitu dukani kwani wote wawili wanaleta faida kwenye kijiji. Kutofautisha kazi ni njia tu ya mgawanyo wa kazi, kwani hata kama kuna kazi nyingine inajulikana wazi kuwa leo inawezekana nikawa kazi ngumu lakini kesho na mimi nitakuwa nafanya kazi rahisi. Mtu habaki kwenye kazi ile ile moja. Hata kama tukigawanyika katika vikosi, vikosi vitabadilishana kazi na hata kikosi changu kama leo kikifanya kazi ngumu kesho huenda kitakuwa katika kazi rahisi. Kwa hiyo kazi zote sharti zipewe siku ile ile moja tu na ziwe na thamani moja.

Bw Mudodo: Kazi ya ujenzi ni ngumu, inatumia akili na nguvu; dukani pia ni kazi ngumu kwani inahitaji mtu akae saa nyingi kushinda hata yule aliyekwenda kulima. Jambo hili tulilijadili na tukaona kuwa kazi zote ni sawa tu. Kwa hiyo kila mtu apewe siku sawa tu.

Bw Nhalima: Mimi pia nadhani kwa sasa njia nzuri ya kufuata ni hiyo ya kupeana siku sawa. Labda hapo baadaye kijiji kitakapokuwa kimeendelea zaidi na kuongeza shughuli zake za uchumi ndipo jambo hili litaweza kubadilishwa. Kama wanakijiji wakiamua kuwa kazi fulani zipewe siku tofauti basi hapo ndipo uamuzi utafanywa.

Bi Pamba: Mimi nadhani itafaa kila mtu apewe siku sawa tu hata kama akienda kufanya kazi ya namna gani. Hapo itakapoonekana kuwa kuna kazi nyingine ambazo ni ngumu zaidi, basi kamati ya kazi itaweza kuziangalia na kubadili utaratibu huu.

Bi Bertha: Mimi pia naona kuwa fundi mwashi na mwuza-duka wana kazi ngumu sana hata kushinda anayekwenda kulima.

Mapolu: Kwa hiyo fundi mwashi na mwuza-duka wapate siku zaidi kuliko anayekwenda shambani?

Bi Bertha: Hapana, wote wapate siku ile ile moja tu.

+++++++++++++++++++++++++++++
+++++++++++++++++++++++++++++

"Mgawanyo wa kazi katika kijiji cha Mbambara, Tanga, ulikuwa kama ifuatavyo wakati fulani:

Kulima mraba wa yadi 140 kwa yadi 4 ni sawa na kukata mizigo 50 ya majani 30 ya mkonge halafu ni sawa na kufanya kazi tangu saa 1.30 asubuhi hadi saa 8.30 mchana katika bustani halafu halafu.... n.k

– B. Wisner, M. Kassami, na A. Nuwagala, "Mbambara: The Long Road to Ujamaa".

# KUANGUSHWA KWA SERIKALI AFRIKA

na

J. Mporogoma

Hadi hii leo Afrika bado ni kilango cha kuchezea mabeberu na mabepari wa kila aina. Uchumi wa Bara la Afrika bado uko mikononi mwa mabeberu, maana umeunganishwa kikamilifu na uchumi wa kibepari wa Ulaya Magharibi na Marekani Kaskazini tangu ukoloni ulipofika katika Bara letu. Bei za mazao ya kilimo ziko chini sana na zinazidi kuteremka mwaka hata mwaka, wakati huo huo mashine na vyombo mbalimbali vitumiwavyo katika nchi zetu na ambazo huagizwa kutoka Ulaya Magharibi na Marekani Kaskazini zinazidi kupanda.

Si jambo la ajabu kwamba hali za maisha ya wafanyakazi na wakulima katika Bara letu zinazidi kudidimia - ingawa ni wafanyakazi na wakulima hawa hawa ndio wanaozalisha utajiri mwingi wa Afrika ambao unatiririka kwenda katika nchi za kibeberu kila saa, dakika, na nukta ipitayo.

Ukweli ni kwamba Waafrika bado hatujapata uhuru wa kweli. Serikali zilizo nyingi hapa Afrika ni vyombo tu vya wakoloni ambao wameondosha bendera zao hapa Afrika lakini bado wanaendelea kututawala na kutunyonya. Katika hali hii, kumetokea katika nchi fulani fulani watu binafsi ambao walikuwa na nia ya kuwatoa wananchi katika janga la kunyonywa na kukandamizwa; watu hawa walimaendeleo wameshindwa kushika hatamu za serikali kwa muda mrefu na shabaha zao zimebaki ni ndoto tu kwa sababu punde si punde serikali zao ziliangushwa na badala yake hatamu zikaangukia katika mikono ya wanyonyaji na wapinga-mapinduzi. Pahali pengine hatua muhimu za kuwakomboa wananchi zimeshindikana kuchukuliwa kwa kuogopa serikali kuangushwa na jeshi.

Kusudi la makala hii ni kuchambua suala hili muhimu la kuangushwa kwa serikali katika Afrika, jambo ambalo limekuwa la kawaida sana siku hizi.

Jambo la kwanza ambalo lazima lieleweke wazi ni kwamba chombo muhimu kushinda vyote katika serikali yoyote isiyo ya kijamaa ni jeshi. Serikali yoyote ya kinyonyaji sharti itegemee nguvu za kijeshi katika kulinda maslahi yake. Kwa hiyo basi jeshi katika mazingira haya nalo lazima liwe ni jeshi la kinyonyaji. Jambo la pili linalotupasa tuzingatie ni kwamba hali ya jeshi lolote lile linategemea kiwango kilichofikiwa na uchumi wa nchi iliyopo jeshi hilo. Nguvu za jeshi hazitegemei fikra au ujanja wa kamanda wake, bali ni kiwango cha ufundi na nyenzo za uzalishaji mali katika kila nchi.

Wakoloni walipotuvamia na kututawala jambo la kwanza walilotunyang'anya ni silaha - yaani uwezo wa kujilinda na kujikinga sisi wenyewe. Inajulikana wazi kwamba Afrika imekuwa na majeshi kwa muda mrefu sana. Hannibal wa Cartago aliweza kupambana na Warumi katika vita vya zama za miaka mia mbili kabla ya kuzaliwa Kristo - yaani kiasi cha miaka karibu elfu mbili iliyopita. Ingawa alishindwa baadaye, askari wake weusi waliweza kuonyesha ushujaa mkubwa sana na ilikuwa mara ya kwanza kwa Warumi kuona tembo wakitumiwa kama magari ya kivita yanavyotumiwa siku hizi.

Vile vile wakoloni walipotuvamia walikuta kuna himaya kuwa: Mali, Songhai, Ashanti, Zimbabwe, Buganda, Abyssinia, Kongo, na kadha wa kadha. Mataifa haya yalikuwa na majeshi yenye silaha imara kulingana na uchumi wake wa wakati huo. Mnamo karne ya kumi na tisa, Chaka - jemadari wa Kizulu - aliweza kuwaonyesha Wazungu ujuzi wa kijeshi wa Mwafrika walipojaribu kuadhiri uhuru wa wananchi. Menoliki wa Abyssinia nayo aliwashinda Waitaliano katika vita vya Assawa mwishoni mwa karne hiyo hiyo ya kumi na tisa.

Kisha, vita vya Maji Maji, vita vya Mkwawa, na kad[illegible] vinaonyesha uwezo wa Mwafrika kupigana kijeshi. Majina Hannibal, Chaka, Meneliki, Lobengula, Mkwawa, Mirambo, ushahidi wa uwezo huu mkubwa. Kwa hivi ni kasumba ya k[illegible] tu ndiyo iliyotufanya kila tunapofikiri juu ya mashuja[illegible] kijeshi tuwakumbuke akina Washington, Nelson, Napoleon, Mazzini, Clausewitz, na wazungu wengine.

Jambo la kuzingatia ni kwamba katika jamii za Kiafr[illegible] mwananchi alipitia katika mafunzo mbalimbali yaliyomtaya[illegible] tu kuishi na wenziwe kama itakiwavyo na jamii bali pia k[illegible] jamii hiyo kama ikipasa. Pindi mtu alipofikia umri ful[illegible] sa afunzwe mila, sheria, kanuni, na historia ya jumuiya wakati huo huo pia alifunzwa ujuzi na hekima za kila ain[illegible] ze kutumikia jumuiya hiyo; na mwisho alipewa ufundi na m[illegible] kishujaa ili aweze kutetea jamii kutokana na mashambulizi adui au wanyama wa mwitu.

Pindi tulipovamiwa na wakoloni, jambo la kwanza tul[illegible] ng'anywa kama tulivyokwisha kusema ni silaha tulizokuwa [illegible] Walitunyang'anya pia utamaduni wetu ili tuwe vinyago vya[illegible] siweze kujihifadhi sisi wenyewe kitamaduni, kiakili, na [illegible] shi. Na mwisho walitunyang'anya uchumi wetu na kutulazi[illegible] kutekeleza maslahi yao ya kiuchumi- yaani kulima mazao [illegible] wao badala ya yale tuliyohitaji sisi wenyewe.

Kwa hivi majeshi ya kikoloni yaliyoanzisha hapa Afri[illegible] kama vile "King's African Rifles" (K.A.R.), "West African Frontier Forces" (W.A.F.F.), na kadhalika yalikuwa na shabaha ya kuthibitisha utawala wa wakoloni zidi ya wananchi. Mafunzo yaliyotolewa katika majeshi haya yalikusudia kumfanya mwananchi awe ni mtumwa wa wakubwa, hakuruhusiwa kufikiri bali kutii tu amri. Ni baadaye tu ndipo hata Mwafrika alipoanza kupewa mafunzo ya uofisa jes[illegible] lakini mafunzo hayo yalikuwa ya kikoloni hasa: walifundish[illegible] mila za Kizungu na ustadi wa kijeshi uliolingana na mahit[illegible] ya kupambana na wananchi wasio silaha - yaani kutuliza gha[illegible] na si kupambana jeshi jingine kutoka nje. Wengi kati ya maofisa hao wa kijeshi waliopikwa wakati huo na ambao ndi[illegible] ngozi wa majeshi mengi ya Afrika ya leo, bado huabudu vyuo kikoloni ambako walipata mafunzo yao: Sandhurst, Mons, St[illegible] West Point, na kadhalika. Ukiangalia sheria zilizopo kati[illegible] jeshi yetu utakuta ni zile zile zilizotungwa katika vyuo h[illegible] ukichunguza uhusiano baina ya askari wa majeshi haya utaku[illegible] kuwa ni ule wa watoaji na wapokeaji amri, ukigeukia mahusi[illegible] baina ya askari na umma utakuta ni yale ya kukandamiza na [illegible] sha wananchi.

Ni kutokana na majeshi ya namna hii ndipo tumepata wa[illegible] kama Ankraha na wenziwe waliomwangusha Kwame Nkrumah na k[illegible] sha nyuma hatua zote za kimaendeleo alizokuwa ameziweka hu[illegible]

Uhuru uliopatikana katika nchi za Kiafrika kusema kwa[illegible] uhuru wa bandia. Serikali mpya zilizoundwa baada ya wakol[illegible] kuteremsha bendera zao zilikuwa ni za vibwanyenye, navyo h[illegible] kukawia kuanza kujilimbikizia mali wakati wananchi walizidi kuteseka na ufukara. Uchumi ulibaki mikononi mwa mabeberu. Muundo wa mashirika yote ulibaki ni uleule wa kikoloni. K[illegible] kweliWazungu wala hawakuondoka, kwani walibaki kama wataala washauri - na mara nyingine hata waandishi-muhtasi na wasai[illegible] wa Marais wetu walikuwa ni Wazungu wale wale waliotunyanyas[illegible] miaka nenda miaka rudi. Majeshi yalibaki ni yale yale yali[illegible] nzishwa na wakoloni: kimuundo, kifikra na hata kisilaha. [illegible] beberu waliona majeshi haya katika nchi zetu tulizoziita h[illegible] vyombo vya maana vya kulindia maslahi yao.

Kutokana na hali hii mambo muhimu ya kuzingatia wakati tukichunguza kuangushwa kwa Serikali yoyote ile ni kama haya: Je, serikali iyo ilikuwa imechukua hatua gani katika kujaribu kuondoa mizizi ya ukoloni inayosalia hata baada ya wakoloni kuteremsha bendera yao? Je, serikali hiyo ilichukua hatua gani kulibadilisha jeshi ili lilingane na matakwa ya wananchi? Je, ni kiasi gani serikali hiyo ilikuwa ikitekeleza maslahi ya wananchi na kiasi gani ilikuwa inapiga domo tu huku uchumi wa nchi ukinyonywa na mabeberu?

Tukizingatia mambo haya tutaona kuwa serikali kama hiyo imeangushwa kwa sababu mojawapo kati ya hizi mbili zifuatazo: Kwanza, serikali hiyo ilikuwa imejaribu kuchukua hatua za kimaendeleo kuwaletea uhuru wa kweli wananchi lakini haikutekeleza hatua hizo kwa njia za kisayansi na hivyo wakubwa wakaweza kutumia jeshi kuing'oa serikali hiyo. Pili, serikali hiyo ilikuwa ni kibaraka wa mabeberu na kuangushwa kwake ni matokeo ya vibaraka kugombana wao kwa wao wakisaidiwa na mabeberu mbalimbali

Hebu tuangalie baadhi ya nchi ambako serikali zimepata kuangushwa.

<u>Misri</u>: Mnamo mwezi Julai mwaka 1952 Mfalme Faraule alipinduliwa na maofisa wa jeshi waliokuwa katika "Umoja wa Maafisa Huru (Free Officers Movement) wakiongozwa na Nagib na A. Gamal Nasser. Misri ilikuwa imezorota, wananchi wengi walikuwa wamebaki kuomba-omba mitaani tu, umalaya ulikuwa juu kabisa, Waingereza ndio waliokuwa mabwana wakubwa. Toka mwaka huo hadi mwaka 1970 Nasser alipofariki Misri ilikuwa imebadilika sura kiasi cha kutosha, baadhi ya njia kuu za uchumi zilitaifishwa, mfereji wa Suez ulitaifishwa pia, na Misri ikaanza kusifika kwa kupendelea siasa isiyofungamana na upande wowote. Ni wazi kuwa jeshi kumpindua Faraule lilikuwa ni jambo la kimaendeleo.

<u>Sudan</u>: Mnamo mwezi Novemba mwaka 1958 Jenerali Abboud alichukua mamlaka mpaka mwaka 1964 ambapo serikali yake naye, ikiwa ni ya kipinga-mapinduzi, ilipoangushwa na jeshi.

<u>Congo</u>: Mnamo mwezi Agosti mwaka 1963 wananchi walimgomea kibaraka Yolou na akaondolewa. Jeshi lilihakikisha kuwa Massemba Debat anakuwa Rais. Mwezi Juni mwaka 1966 kulikuwa na majaribio ya kumwangusha Debat kwa sababu alianza kuzungumzia "Bantu Socialism". Mwezi Septemba mwaka 1968 Kapiteni Raoul alichukua madaraka na baadaye Moja Ngouabi akawa Rais.

<u>Ghana</u>: Nkrumah alikuwa ni mwananchi wa kimaendeleo na aliweza kuifanya nchi yake iwe miongoni mwa makoloni ya kwanza katika Afrika kujipatia uhuru wake hapo mwaka 1958. Alizungumza juu ya ukombozi na umoja wa Bara lote la Afrika na juu ya Ujamaa na maendeleo nchini mwake. Lakini hakubadili muundo wa jeshi la nchi yake na akawa amezungukwa na mabwanyenye waliowapa vyeo mbalimbali. Aliangushwa na jeshi mwezi Februari mwaka 1966 na vibaraka Afrifa na Ankrah wakashika madaraka wakiwa pamoja na Mkuu wa Polisi, Harlley. Hawa walibadili siasa ya Ghana na nchi hiyo ikarudi katika ukoloni mamboleo. Luteni Arthur alijaribu kuiangusha serikali hiyo mwezi Aprili mwaka 1967 lakini alishindwa. Kanali Acheampong aliiangusha serikali hiyo hapo mwaka 1971.

<u>Sierra Leone</u>: Mnamo mwezi Machi mwaka 1967 Luteni Kanali Smith aliiangusha serikali ya Albert Margai. Mwezi Aprili mwaka 1968 askari wa kawaida waliiangusha serikali ya kijeshi na kumruhusu Siaka Stevens kuunda serikali - yeye alikuwa amezuiwa na yule Luteni - Kanali ingawa alikuwa ameshinda uchaguzi.

<u>Libya</u>: Mwezi Septemba mwaka 1969 Mfalme Idris aliangushwa na Baraza la Mapinduzi likiongozwa na Kanali Moumar Ghaddafi.

............./

Somali: Mnamo mwezi Oktoba mwaka 1969 serikali ya Somali Youth League iliangushwa na Baraza la Mapinduzi likiongozwa na Jenerali Siad Barre.

Mali: Mnamo mwezi Novemba mwaka 1968 Modibo Keita aliangushwa na jeshi kutokana na siasa yake ya kimaendeleo na nia yake ya kuwa na jeshi la mgambo licha ya jeshi la kawaida. Luteni Traore alichukua madaraka.

Zaire: Mwanzoni mwa mwaka 1960 Jenerali Mobutu alimwangusha mwanamapinduzi mkubwa, Ndugu Patrice Lumumba aliyekuwa akitaka uchumi wa Zaire uwanufaishe wananchi wa nchi hiyo hiyo. Mobutu alitumiwa na mabeberu ambao wana raslimali nyingi sana katika nchi hiyo.

Ethiopia: Mwezi Desemba mwaka 1960 kulikuwa na jaribio la kuangusha Mfalme Haile Selassie lakini halikufaulu.

Nchi zifuatazo chini nyingi ni makoloni zamani ya Ufaransa. Majeshi yalikuwa yakizing'oa serikali katika nchi hizi ili watu mbali mbali nao wapate kuiba fedha - kila mwanajeshi anaenda Ikulu, anaiba fedha nyingi kadiri awezavyo, halafu anaangushwa na mwingine naye anakuja kufanya hivyo hivyo wakati wale walio wanastarehe huko Ulaya; wananchi ikiwa ndio wanaopata hasara tu: Dahomey, mwaka 1963 Kanali Soglo alimwangusha H. Maga; mwaka 1967 Soglo aliangushwa na Kanali Alley; na vivyo hivyo. Gobon, mwaka 1964 majaribio ya kuangusha serikali yalifaulu lakini Wafaransa wakaingilia kati ya kurudisha serikali ya kwanza. Burundi, mwaka 1965 maofisa wa kijeshi walimpindua Mfalme Mwambutsa, mwaka 1966 Micombero alitwaa madaraka. Jamhuri ya Afrika ya Kati mwaka 1966 Kanali Bokassa alimwangusha David Dacko. Upper Volta, mwaka 1966 Kanali Lamizana alimwangusha Yameogo. Katika Nchi za Niger, Senegal, Ivory Coast majeshi ya lakini hayakufanikiwa.

Nigeria: Mwezi January mwaka 1966 General Ironsi alimwangusha Sir Tafawa Balewa; mwezi Julai mwaka huo huo Ironsi aliangushwa na Jenerali Yakubu Gowon.

Uganda: Mwanzohi mwa mwaka 1971 Obote aliangushwa na Jenerali Amin

Togo: Mnamo mwezi Januari mwaka 1963 Sylvanus Olyimpio aliangushwa na Grunitzky.

Inatupasa kwa sasa tuanze upya kutazama hali ya Afrika kwa macho makali, akili zetu tuzinne. Sharti tuelewe vyema wapi tunatoka, wapi tumefika, na wapi tunakwenda. Ni wazi kabisa k majeshi tuliyorithi, kama ilivyo kwa upande wa uchumi, bado ha Karibu laki sita ya Waafrika ni wanajeshi, kati ya hao maofisa wamesomea nchi za nje. Hata baadhi ya vyuo vilivyoanzishwa k ni vivuli vya vyuo vilivyoanzishwa katika nchi za kibeberu. N nyingi za Kiafrika zinatumia fedha nyingi kwa ajili ya majeshi wakati wananchi hawana chakula. Bado majeshi hayashiriki kati uzalishaji mali, wananchi hawana silaha.

Hali hii inaleta kunyonywa na kunyanyaswa kwa Mwafrika.

**************

TAARIFA YA SAFARI YA
UNGUJA

Madhumuni ya safari:

Madhumuni ya safari hii yalikuwa ni kwenda kusherehekea siku Kuu ya kuanzishwa kwa Chama cha Afro Shiraz Party tarehe 5 Februari, ambacho ndicho chama kitukufu kilichomkomboa Mwafrika Unguja.

WALIOKUWAPO:

Ndugu Kakwezi (Bi)
" Lwambo " "
" Kileo " "
" Jumbe
" Mhilu
" Mulokozi
" Mahinja
" Tarimo

Safari ilianza siku ya Jumatatu jioni tarehe 30/1/73. Wajumbe hao hapo juu tukisindikizwa na Ndugu C.C. Liundi Mwenyekiti wa T.Y.L. Wilaya ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, tulikwenda mpaka bandarini Dar es salaam ambako tulijiunga na vikundi vya wasafiri wengine kuingoja meli ya kutuchukua.

Bandarini tuliungana na vijana kutoka Chuo Kikuu cha Makerere, tukawa kundi moja la Wanafunzi. Kwa bahati mbaya meli haikufika mpaka kesho yake asubuhi.

Kesho yake asubuhi tarehe 1/2/73 meli ya Jamhuri ambayo ni meli ya Serikali ya Unguja iliwasili, na sisi wote tukaiabiri tayari kwa safari.

Ilipotimia saa 3 asubuhi tarehe hiyo hiyo safari ilianza ikiongozwa kwa ujumla na Ndugu Shija, Naibu wa Katibu Mkuu wa Vijana Tanzania Bara.

UNGUJA

Tulifika Unguja kunako saa 8 mchana tarehe hiyo hiyo ya 1/2/73. Huko tulilakiwa vizuri sana na wenyeji wetu. Muda mfupi tu baada ya kulakiwa tulipelekwa kwenye jumba la Majilis Kuu ya Zamani, ambako wageni wote walikuwa wanakaribishwa.

Baada ya kupumzika kidogo kikundi chetu cha wanafunzi-ambacho kilikuwa na watu 11 kilichukuliwa kwenye gari na kupelekwa shule ya Ufundi ya Mbweni, ambako tulipewa vyumba vyetu tulirudishwa mjini Zanzibar.

Mjini Zanzibar tulikula na kulitalii jiji kwa muda uliobakia katika siku ile. Jioni tulikuwa tumechoka tukarudisha Mbweni kulala.

TAREHE 2/2/73

Siku hii tulipangiwa viongozi wetu wa kutuongoza kwenda katika sehemu mbali mbali za Unguja. Pia tulionyeshwa gari ambalo lingeshughulika na shughuli za usafiri za kikundi chetu.

Baada ya shughuli hiyo tulipewa tena fursa ya kulitalii jiji la Zanzibar.

TAREHE 4/2/73

Asubuhi tulikwenda Ikulu kuonana na Mwenyekiti wa Afro Shiraz Party, Mheshimiwa Aboud Jumbe. Huko Ikulu vijana wa Chuo Kikuu cha Makerere walisoma risala waliyokuwa wamekuja nayo kwa Mwenyekiti wa A.S.P. Baada ya risala kusomwa Mheshimiwa Aboud Jumbe alizungumza nasi kwa muda mfupi juu ya mapinduzi ya kote Tanzania Kisiwani, na Bara.

Baada ya Mazungumzo kikundi chetu kilikwenda kwenye kiwanda cha kutengeneza viatu kwa makusudi ya kudaidia kazi.

Jioni ya siku hii tulihudhuria kwenye sherehe za michezo y
Ngoma, iliyokuwa ikichezwa na vikundi vitano (5) vilivyochaguli,
kutoka katika Tanzania nzima, na kutoka Frelimo pia.

**TAREHE 5/2/73**

Siku hii ndiyo iliyokuwa upeo wa sherehe mjini Zanzibar na
Unguja nzima. Asubuhi tuliandamana kwa vigelegele vya shangwe n
furaha kwa kukumbuka kuanzishwa kwa chama kitukufu cha A.S.P.
Mwisho wa maandamano Mheshimiwa Mwenyekiti wa A.S.P. Bwana Aboud
Jumbe aliuhutubia Mkutano.

Katika hotuba yake alieleza historia ya A.S.P. na vikwazo
mbali ambavyo ilibidi ivipitie mpaka ikaweza kumkomboa mnyonge U
Kwa kumalizia hotuba yake aligawa kazi ya kuandika historia ya
A.S.P. kwa vikundi mbalimbali wakiwemo vijana wa Young Pioneers,
Jeshi la Polisi, jeshi la Ulinzi, Umoja wa wanawake na Idara
mbalimbali za A.S.P.

Mchana wa tarehe hii tulikwenda kuona michezo ya halaiki
iliyokuwa ikifanywa na vijana Watanzania wapatao 5000 hivi.

Usiku wa tarehe hii tulitazama mchezo wa mpira uliokuwa
ukichezwa kati ya timu ya Unguja na Zambia.

**TAREHE 7/2/73**

Baadhi yetu tulikwenda Unguja shamba kuona maendeleo mbalim
yaliyofanywa na wanavijiji. Huko tuliona vijiji vya Ujamaa
vinavyostawi, kimojawapo kikiwa ni Chanani. Halafu tukaona shamb
Serikali la Mpenja, mwisho tulikitembelea kijiji cha Bumbi, ambac
ni kijiji chenye historia ya peke yake na ya kuvutia katika siasa
ya Unguja.

**TAREHE 8/2/73**

Tulijitayarisha kwa safari ya kurudi Tanzania Bara, na kuna
saa 4 asubuhi sehemu moja ya kundi letu iliingia katika ndege na
Dar es Salaam. Kundi lililobakia lilipata ndege kwenye saa 7.30
pia likarudi Dar es salaam.

**MAONI YETU**

Mambo makubwa ambayo tuliyaona Unguja ni Mwamko wa Siasa wa
Maendeleo ya mtu wa Kawaida, na hali ya amani na utulivu wa nchi

Kuhusu Mwamko wa siasa tungependa kusema kwamba huko kisiwa
mtu yu macho. Po pote mgeni apitapo unaweza kuwa na hakika kwamb
unachunguzwa na ikiwa wewe ni mgeni adui kushikwa na mtu wa kawai
jambo rahisi sana.

Kwa upande wa maendeleo ningependa kusema kwamba unguja ik
mbele yetu sana. Watu wa hali ya chini kiuchumi, wakisaidiwa na
serikali ya mapinduzi na kuongozwa na A.S.P. wamepiga hatua kubwa
sana mbele. Watu kwa kushirikiana wamejijengea majumba mazuri ya
Serikali ya mapinduzi haikusita kuingiza maji na umeme katika maj
hayo. Wanacholipia wananchi ni maji na umeme tu, na hata hivyo
hawawezi kudaiwa zaidi ya shilingi 30/= kwa mwezi kwa jamii moja.

Mwisho ningependa kusema kwamba visiwa vya Unguja viko shwa
sana, na yeyote aingiaye katika visiwa hivyo atajua tu mara moja
ni nchi ya watu wenye amani, waliotulia na wenye kuhoshimiana.
na uhuni Unguja ni mwiko.

Joseph A.L. Tarimo
KIONGOZI WA SAFARI

## MWANGALIE MKULIMA

na

M.M. Mulokozi

1. Mwangalie mkulima akichimba
Anapasua udongo na miamba,
Magugu na mabuu anayakumba
Na mwishowe haambulii kibaba.

2. Mwangalie mwalimu anavyocheza
Pamoja na watoto anaofunza,
Ona anaviringika kama chenza
Hajui hatima ya anaofunza.

3. Mwangalie kiongozi na kelele,
Sauti aipaza hata kilele,
Jasho lamdondoka kama mchele -
Apigana taifa lisonge mbele!

4. Mwangalie kuli alivyojipinda,
Mgongo kaupakia kama punda,
Hivyo hivyo kutwa nzima anatanda,
Fungule kashuka, hawezi kupanda.

5. Mwangalie Singh na jiduka lake,
Anayumbayumbisha kitambi chake,
Basi lile pale ati mali yake
Na lile kasiri ni kozia yake.

6. Mwangalie yule mtoto rijale,
Si miaka miwili katoka shule;
Achumile bwana mashahada tele -
Hadondoshi jasho, benzile li pale

7. Naam, watazame wote na kisha
Tafiti tena ramani ya maisha:
Shangwe za Uhuru sasa zimekwisha -
Kilichosalia kejeli komesha!

*******

"Kuna nchi sasa zinazojitawala katika Afrika, na kuna namna mbali mbali za kutawala. Ya kwanza watu wanakabidhiwa madaraka kundi dogo, ndio hawa kina sisi hapa tunaoitwa wanasiasa. Hili kundi la wanasiasa nchi yoyote haliwi kundi kubwa. Kuna jingine dogo linaitwa la watumishi wa serikali, halikadhalika huwa kundi dogo; halafu jingine dogo ni la jeshi pamoja na polisi. Basi njia moja ya kutawala ni kuungana vikundi hivyo vitatu na kuunda chama cha kutawala. Na ikisha kuwa hivyo wakulima na wafanyakazi hawana chao, hawana pa kupenya. Wanasiasa hao na wenye silaha na mabingwa wote wakiunda chama chao kimoja cha kutawala huwa chama cha wanyonyaji wakubwa; wakulima, wafanyakazi hawana pa kufurukuta tena. Nchi ya namna hiyo wanyonyaji wanaiita nchi isiyokuwa na wasiwasi, au kwa Kiingereza, stable."

Mwalimu J.K.Nyerere

*******

# RIPOTI YA SAFARI YA CHUNYA

MADHUMUNI.

Kwa muda mrefu tumependa kupata nafasi ya kuyaweka katika vitendo yale ambayo tunajifunza kinadharia. Kwa vile tumaini kubwa la maendeleo katika nchi hii limo katika kilimo, tuliona ni bora tutumie sehemu ya likizo yetu katika vijiji ambavyo vinashughulika zaidi na ulimaji wa mazao mbalimbali.

Kuchaguliwa kwa wilaya ya Chunya kulisababishwa zaidi na taarifa ambayo Mwenyekiti wa Taifa wa Vijana wa TANU, Ndugu P. Qorro, alitoa alipotembelea vijiji vya wilaya hiyo. Chunya ni wilaya mojawapo (kama si pekee) ambayo vijana wamalizao masomo ya shule za msingi na hawakupata bahati ya kwenda mbele zaidi, humezwa katika vijiji vya ujamaa. Ikiwa vijana hao hawashughuliki na utafutaji wa kazi maofisini, ni vipi basi wameshikwa na wito huo? Ni katika kuona, kuhisi na kupata jawabu hilo tukaenda huko Chunya.

Safari ilipangwa na kutayarishwa na makao makuu ya vijana wa TANU na usimamizi wa shughuli zote ulikuwa wao.

Kwa watu wengi neno Chunya litawakumbusha mahali ambapo wakati wa ukoloni dhahabu nyingi ilikuwa inapatikana, dhahabu ambayo kwa namna moja au nyingine imejenga Mbeya na Iringa - ukiachilia mbali utajiri mwingi uliotoka nje ya mikoa hiyo, na hata nje ya nchi hii. .Ni picha ya namna hiyo tu inayobaki kwa wengi.

Kutokana na unyonyaji huu/tajiri wa wilaya pia kwa sababu ya ukame wa nchi wenyeji - Wambungu, Wakimbu na Waguruka - mara kwa mara walikuwa wanapatwa na baa la njaa. Serikali ilikuwa inatumia fedha nyingi kuwalisha watu. Jitihada hii haikuwa ni dawa kwani mzizi wa shida haukuwa umeshughulikiwa.

OPERESHENI CHUNYA

Mwaka 1972, Operesheni Chunya ilianzishwa katika wilaya hii. Kabla ya mpango huu kuanzishwa, serikali ilikuwa kila mwaka inatumia kiasi cha Sh. 400,000/= kuwalisha wananchi. Hivyo basi Operesheni Chunya ni mpango maalum wa kimaendeleo katika kuwashawishi wananchi ili wakae pamoja na kufanya kazi pamoja kuondoa tatizo la njaa na kuinua hali ya uchumi.

Ardhi: Wilaya ya Chunya ambayo eneo lake ni maili za eneo 10000 ina ardhi bora sana kwa mazao ya pamba na tumbaku. Ni [illegible] katika wilaya hii peke yake katika Mkoa wa Mbeya ambako mazao hayo yanastawi zaidi.

Hali ya Asili: Wilaya hii ina misitu ambayo nyuki hupatikana kwa wingi, hivyo inafuata kuwa asali na nta, mazao ambayo ni ya thamani, hupatikana. Mininga ambayo hutoa mbao hupatikana kwa wingi. Miti mingine ambayo hufaa kwa mkaa na matumizi mengine ipo pia. Wanyama wa porini, kama tembo, wanapatikana kwa kiasi kikubwa.

Ziwa Rukwa, ambalo ni ziwa mojawapo linalotoa samaki kwa wingi katika Tanzania lipo katika wilaya hii. Samaki wa ziwa hili wanauzwa kwa wingi nje ya Mkoa wa Mbeya; kama vile Mikoa ya Ruvuma, Lindi na Mtwara.

MATATIZO YA AWALI

Kama ilivyoelezwa hapo juu karibu kila mwaka fedha kiasi kikubwa zilitumika kuwalisha wananchi. Kwa sababu ya kuingiliwa [illegible]

na "[illegible] kwa utani waliita Chunya "Wilaya iliyolaaniwa na Mungu! Kulikuwa na sababu zilizofanya njaa isihame kabisa humo wilayani. Wenyeji wa wilaya hii - Wakimbu, Wambungu na Waguruka - hukaa mbalimbali; hivyo huwa vigumu, siyo kwao tu kulima kwa kushirikiana bali pia kwa upande wa serikali kutoa uongozi juu ya kilimo bora. Wananchi kwa hiyo, kutokana na hali hiyo, walilazimika kutumia kilimo cha jadi. Uhaba wa mvua kwa sehemu kubwa ya Chunya hufanya mavuno yapatikanayo kila mwaka kwa mtindo huo wa kilimo kuwa machache! Mazao machache yaliyokuwa yanapatikana yalishambuliwa na baa jingine, nguruwe, tembo na panya.

Pamoja na matatizo hayo uendelezaji wa kilimo ulitatizwa na "usekesaji". Itakumbukwa kuwa wilaya hii ilikuwa inatoa dhahabu nyingi katika nchi hii. Umaarufu wa migodi hiyo ulivuta watu wa sehemu mbali mbali, si kutoka Afrika ya Mashariki tu, bali pia nje yake. Inasemwa kuwa hadi leo hii, Chunya (mjini) kuna watu ambao asili yao ni makabila mengi ya Afrika. Migodi ilipofungwa mabepari waliwaajiri watu wengine kutafuta dhahabu katika vijito, na tendo la namna hiyo ndilo linaloitwa "usekesaji". Shughuli hii kwa kawaida huanza wakati ule mvua zinapoanza (kwa vile ardhi huwa si ngumu, na ni wakati ule ule ulimaji huanza kwa nguvu. "Wasekesaji" hurudi nyumbani mvua zinapokatika.

<u>OPERESHENI CHUNYA</u> ilikuwa katika hatua kuu tatu:

1. Mwaka 1972/73: Lengo kuwa na watu 5000 katika vijiji vya Ujamaa
2. Mwaka 1973/74: Lengo - kuwa na watu 10, 000 katika Vijiji vya U.
3. Mwaka 1974/75: Lengo: Wananchi 15,000 katika Vijiji vya Ujamaa.

Lengo la Kipindi cha 1 na cha 2 lilivukwa katika Kipindi cha 1 tu.

Vijiji ambavyo vimepiga hatua zaidi ni Kipembawe, Mwambani juu na Gua, ambavyo hulima zao la tumbaku. Mwaka 1972, kijiji cha Gua kilikuwa juu katika vijiji vyote vya Mkoa wa Mbeya.

<u>KIJIJI CHA UJAMAA, GUA</u>

Kijiji hiki kimegawanyika katika sehemu mbili: Gua A na Gua B. Gua A kuna mchanganyiko wa wazee na vijana. Gua B ni vijana watupu.

<u>Historia.</u> Gua A kilianzishwa rasmi tarehe 1/8/70, kikiwa na wanakijiji zaidi ya 100. Baadaye idadi hii ilipungua, wakabakia wakulima 81 tu na jamaa zao.

Matatizo.

<u>Mahudhurio</u>; Mwanzoni mahudhurio ya wanakijiji kazini hayakuridhisha. Kwa sababu ya umbali mkubwa kati ya kijiji na makazi yao ya kawaida. Tatizo hili lilitatuliwa kwa kujenga nyumba za muda katika eneo la kijiji.

<u>Upungufu wa Mvua:</u> Sababu ya ukosefu wa mvua, kuna ukosefu wa maji. Wakati mwingine hubidi tumbaku imwagiliwe maji toka kijitoni - kwa ndoo! Gua ni miongoni mwa vijiji vitakavyopewa msaada wa maji na serikali siku za karibuni.

<u>Upungufu wa Wataalam:</u> Mwanzoni kijiji hakikuwa na wataalam wa kilimo, ufugaji, n.k. wa kuwashauri wanakijiji. Hivi sasa kijiji kinao wataalam zaidi ya 13, wakiwemo walimu 5, waganga wasaidizi 3, mabwana shamba 3, n.k.

<u>Kitoweo:</u> Hili ni tatizo kubwa katika kijiji hiki cha Gua. Kwa sababu ya mbung'o, ufugaji wa ng'ombe hauwezekani. Aidha, kwa sababu ya ubovu wa mawasiliano ni vigumu kuleta samaki toka Ziwa Rukwa. Walakini wanyama mwitu ni wengi katika eneo la kijiji. Hivyo kwa msaada wa serikali wanakijiji wangeweza kulishinda tatizo hili kwa kuruhusiwa kuwinda wanyama wa mwitu kwa ajili ya kitoweo. Aidha ufugaji wa mbuzi na kuku ungesaidia.

GUA B: Hiki ni kijiji cha vijana watupu kilichoanzishwa mwaka 1972. Kinao wakazi 23. Wengi wao wamehitimu darasa la 7. Gua A & B

kushirikiana huduma za kijiji, mipango ya maendeleo, n.k. ila tu kulima kulima mbalimbali. Gua B mashamba yote ni mali ya kijiji. Gua A, mbali na mashamba ya kijiji kizima, kila jamaa inacho kipande chake cha ardhi ambapo hujilimia mazao ya chakula.

Uchumi: Kijiji cha Gua kinazo shughuli 3 za uchumi: kilimo, ufugaji wa nyuki na duka.

Kilimo: Zao kuu la biashara ni tumbaku. Kutokana na tumbaku, msimu 1970/71 kijiji kililima ekari 21 na kupata jumla ya Sh. 29,752/10. Msimu 1971/72 zililimwa ekari 21, mapato yakawa Sh. 21,983/40. Vijiji vyote pamoja vilitazamia kupata Sh. 53,860 katika msimu wa 1972/73. Lakini kwa bahati mbaya upepo uliharibu sehemu kubwa ya shamba lao; kadhalika mabani 2 ya kukaushia tumbaku yaliungua. Inakadiriwa kuwa hasara iliyotokana na ajali hizi haipungui Sh. 46,075/=.

Chakula: Mazao ya chakula ni mahindi, ulezo, maharagwe, karanga na mihogo. Mpango wa kuanzisha ufugaji wa kuku upo mbioni.

Ufugaji wa Nyuki: Hii ni shughuli ya tangu jadi na jadudi katika Wilaya ya Chunya. Ili kuendeleza ufugaji huu, serikali imewapa wanakijiji msaada wa utaalam wa nyuki na mizinga ya kisasa 180.

Shughuli zinginezo: Kijiji kinayo kwaya yake chenyewe. Kisomo chenye manufaa hufundishwa saa za jioni. Ipo pia shule ya msingi, ambayo, licha ya kuhudumia kijiji, huhudumia pia wananchi wanaoishi ujiranini.

Shughuli Zetu katika Kijiji

Tarehe:

| | | |
|---|---|---|
| 22/3/73 | - | Kuwasili Chunya, alasiri. |
| 23/3/73 | - | Mkutano na viongozi wa wilaya. Mpango wa safari ya kwenda Gua. |
| 23/3/73 | - | (saa 12 jioni) Kuwasili kijijini Gua. |
| 24/3/73 | - | Kuchuma na kuchanganua tumbaku katika shamba la vijana (Gua B.) (Asubuhi hadi saa 6) Alasiri: Kusaidia kazi katika shamba la vijana. |
| 25/3/73 | - | Jumapili. Kung'oa mashina ya tumbaku katika shamba la vijana. |
| 26/3/73 | - | Kusaidia kazi katika shamba la wazee. Vikuudi 4: Kikundi cha 1 kilikwenda kwenye nyuki. Kikundi cha 2 kilichanganua tumbaku kavu. Kikundi cha 3 kilifunga tumbaku katika marobota tayari kwa kuuzwa. Kikundi cha 4 kilichuma tumbaku. |
| 26 - 30/3/73 | - | Shughuli mbali mbali za kijiji, hasa zinazohusu tumbaku. |
| 30/3/73 | - | Kuagana rasmi na wanakijiji. |
| 31/3/73 | - | Kuondoka Gua, saa 1 asubuhi. Njiani tulitembelea vijiji vya Ujamaa vya Kapalala na Mwambani. Jioni: Tafrija ya maagano kwenye makao makuu ya wilaya ya TANU iliyoandaliwa na TYL. |
| 1/4/73 | - | Kuondoka Chunya saa 3 asubuhi. |
| 2/4/73 | - | Kuwasili Dar es Salaam, saa 11 jioni. |

ORODHA YA WALIOSHIRIKI KATIKA SAFARI HII

| | | | |
|---|---|---|---|
| Ndugu | Liundi, C.C. | Ndugu | Thonya, W.B. |
| " | Munga, M.M. | " | Msanganzila, J. |
| " | Mwanga, L. (Bi.) | " | Tibaijuka, C.C. |
| " | Minja, F. | " | Mgeni, B. |
| " | Bura, A. | " | Mulokozi, M.M. |
| " | Matango, R.R. | | |

Ripoti hii imetayarishwa na Ndugu Munga,M.M. &

## SHAIRI: VIJANA WA VIJIJINI

Lilitungwa na Mwenyekiti wa Kijiji cha Ujamaa cha Kapalala 0
Ndugu M. Simba
Kuwakaribisha vijana toka Chuo Kikuu.

=============

Vijana tumeamua, heri kuwa vijijini,
Karibuni e vijana, muone wilaya hii,
Mambo yanavyofanyika, na vijana vijijini,
    Vijana wa vijijini, kazi tunaimiliki.

Wilaya yetu ya Chunya, kweli inajivunia,
Kwa kazi wanoifanya, wa vijijini vijana,
Jembe walishikiliya, kwa moyo mmoja nia,
    Vijana wa vijijini, kazi tunaimiliki.

Kweli jama nawambia, sisi vijana wenzenu,
Wito tumesha itika, wa Raisi baba yetu,
Azimio la Arusha, tumetekeleza kwetu,
    Vijana wa vijijini, kazi tunaimiliki.

Siyo kuwa nadanganya, au kuwa ninazua,
Ninasema la murua, la ukweli kila njia,
Uumeona kwa hakika, jinsi yanavyotendeka,
    Vijana wa vijijini, kazi tunaimiliki.

Kufyeka au kukata, siyo kazi ya kujali,
Kalamu zetu ni shoka, misitu yetu sisi,
Jembe nikishikilia, utanisahau kweli,
    Vijana wa vijijini, kazi tunaimiliki.

Utamaduni ni ngoma, tunacheza vijijini,
Jadi zetu kuzikuza, zilizoachwa zamani,
Elimu ya manufaa, nayo twafanya jamani,
    Vijana wa vijijini, kazi tunaimiliki.

Kuzurura mitaani, hilo jambo hatutaki,
Kwetu linaleta sobi, na maasha ya kiwizi,
Heri kuwa vijijini, kuliko kwenda ngomeni,
    Vijana wa vijijini, kazi tunaimiliki,

Ingawa mwanzo jamani, lakini twajitahidi,
Kumufukuza adui, masikini wilayani,
Jembe na shoka jamani, ni silaha kwetu sisi,
    Vijana wa vijijini, kazi tunaimiliki.

Vijana tuko imara, kusikia viongozi,
Wanalolisema mara, haraka twalikariri,
Nahakikisha imara, Chunya sasa yanawiri,
    Vijana wa vijijini, kazi tunaimiliki.

Sauti imenishia, beti kumi zinatosha,
Samahani nawaomba, Ikiwa nimekosea,
Wallahi bila kuficha, shairi nalimaliza,
    Vijana wa vijijini, kazi tunaimiliki.

KWA NIABA YA UMOJA WA VIJANA WA TANU, WILAYA YA CHUNYA.

NGONJERA YA KUWA KARIBISHA CHUNYA VIJANA TOKA CHUO KIKUU, DAR

Watungaji: Edigard K. Elias (Adili)
Apollonalli Mgaya (Mwadilifu)

Toka Chunya Kati.

Sijui niseme nini, mjue furaha yetu,
Kuwaona mbeleni, kutujia Chunya yetu,
Muingie mpaka ndani, muone vijiji vyetu,
Karibu Chunya, karibu, wageni wetu wanana.

Fikeni na wote wema, muone tulipofika,
Ziara yetu ni njema, wote tunaisifia,
Twatoa zetu heshima, kuona mmeingia,
Karibu Chunya karibu, wageni wetu wanana.

Hakika twasifieni, TANU yetu usukani,
Yaendesha kwa amani, hakika tumo mwangani,
Yatukimbiza nuruni, hatua zetu mbeleni,
Karibu Chunya karibu, wageni wetu wanana.

TANU yetu ni azizi, wote tunaiamini,
TANU yetu ni hirizi, twakubali kwa makini,
TANU yetu ndio mwezi, imetuweka mwangani,
Karibu Chunya karibu, wageni wetu wanana.

TANU pote yasifika, kuenezwa na vijana,
Twaiombea fanaka, usiku kucha mchana,
Tumesha ondoa shaka, tu tayari kuungana,
Karibu Chunya karibu, wageni wetu wanana.

Vijana tu askari, vijiji tutaviunda,
Kupe nao mabepari, vijana budi kushinda,
Siasa yastahiki, bwanyenye hawezi shinda,
Karibu Chunya karibu, wageni wetu wanana.

Qorro hatukumsaza, kumpa zetu shukrani,
Kutuongoza vijana, kutupa yake maoni,
Umoja uliofana, vijana twajivunia,
Karibu Chunya karibu, wageni wetu wanana.

Lengo letu hapa Chunya, ni hali bora za watu,
Juhudi tumeifanya, kuinua uchumi wetu,
Wavivu tunawakanya, waingie lengo letu,
Karibu Chunya karibu, wageni wetu wanana.

Hapa Chunya mnaona, juhudi imefanyika,
Operesheni mwaona, kwa kweli imejengeka,
Maendeleo yafana, Chunya imesha tukuka,
Karibu Chunya karibu, wageni wetu wanana.

Inaeleza ya kazi, sisi tunayoamini,
Iwe ndiyo kiongozi, msingi wa vijijini,
Ni matendo ya azizi, aloleta SELEMANI,
Karibu Chunya katibu, wageni wetu wanana.

Wageni mmesikia, iliyobaki kutenda,
Ujamaa kuinua, tupate bora matunda,
Kutimiza kuwezia, ni bora siyo vinanda,
Karibu Chunya karibu, wageni wetu wanana.

Vibwebwe tumejifunga, kuelekea vijijini,
Kwa pamoja twajiunga, kilimoni mashambani,
Mkoa wetu kujenga, kwa ushirika mwanzoni,
Karibu Chunya karibu, wageni wetu wanana.

(Linaendelea)

Wajibu wetu vijana, ni kulinda nchi yetu,
Yatubidi kukazana, kuinua nchi yetu,
Na vijana ndio sana, kusaidiana kiutu,
Karibu Chunya karibu, wageni wetu wanana.

Tunazo kazi nyingine, za kwendeleza kilimo,
Tusiwachie wengine, kujenga yaso kikomo,
Maadui tuwachane, na Umoja uwe somo,
Karibu Chunya karibu, wageni wetu wanana.

Vijana tuwe ni nguzo, ya kwendeleza usawa,
Umoja wetu si gumzo, ila kwetu ndiyo dawa,
Ujamaa uwe funzo, wanyonyaji waduwaa,
Karibu Chunya jaribu, wageni wetu wanana.

Na pia tuna majonzi, baba yetu katuaga,
Karume wa mapinduzi, buriani kajitenga,
Kafanya mambo azizi, manani ampe mwanga,
Karibu Chunya karibu, wagenu wetu wanana.

Twashukuru kuja kwenu, kutuona hapa Chunya,
Enyi watoto wa TANU, msije kuwa kimiya,
Mkisha kurudi kwenu, msitusahau Chunya,
Karibu Chunya karibu, wageni wetu wanana.

Uhuru tumesha pata, lililobaki kulinda,
Wananchi tuwe kuta, vibaraka kuwawinda,
Ukoloni kuufuta, makupe tutawaponda,
Karibu Chunya karibu, wageni wetu wanana.

Kaditama nakomea, mjamaa nasimama,
Mabwanyenye kuzuia, imara nitasimama,
Viongozi na raia, ki-mapinduzi tu ima,
Karibu Chunya karibu, wageni wetu wanana.

==========

Tungo hizi ni mifano tu ya mlipuko mkuu wa kiutamaduni na msisimko wa kisiasa ulioenea katika vijiji vya ujamaa vingi nchini, hususa katika wilaya zilizosonga mbele zaidi kimwamko kama ilivyo wilaya ya Chunya. Mashairi haya hayakutungwa na "wataalam" au wanazuoni wanaizi wa kunga za utunzi, bali wananchi wenyewe wanaoishi vijijini. Huu ni mfano tu wa Fasihi ya Umma yenye kutetea maslahi ya Umma. Na hii ndiyo jadi asilia ya ushairi wa Kiswahili na Fasihi ya Kiafrika kwa jumla.

- MHARIRI.